# CHIMBUKO LA DHIKIRI: MABADILIKO NA ATHARI ZAKE KWA JAMII YA WAZANZIBARI

Na

Makame Pandu Khamis

Tasnifu Iliyowasilishwa kwa Ajili ya Kukamilisha Masharti ya Shahada ya Uzamili Katika Fasihi ya Kiswahili ya Chuo Kikuu cha Dodoma

Chuo Kikuu cha Dodoma

Oktoba, 2016

## ITHIBATI

Aliyesaini hapa chini anathibitisha kwamba amesoma na anapendekeza tasnifu hii inayoitwa *Chimbuko la dhikiri: Mabadiliko na Athari zake kwa Jamii ya Wazanzibari* ikubaliwe kwa minajili ya kutunukiwa shahada ya uzamili katika Fasihi ya Kiswahili ya Chuo Kikuu cha Dodoma.

**…………………………………**

**Dkt. Muhammed Seif Khatib**

**(Msimamizi)**

**Tarehe…………………**

**IKIRARI**

**NA**

**HAKIMILIKI**

Mimi, **Makame Pandu Khamis**, nathibitisha kwamba tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe halisi na haijawasilishwa wala haitawasilishwa katika Chuo Kikuu kingine chohote kwa ajili ya kutunukiwa digrii nyingine yoyote.

**Sahihi……………………………………**

Hairuhusiwi kuzalisha au kunakili wala kusambaza sehemu yoyote ya tasnifu hii, kwa namna yoyote ile, bila kibali cha mwandishi kutoka kwa mwandishi au Chuo Kikuu cha Dodoma.

**SHUKRANI**

Kazi hii imekamilika kutokana na michango ya watu mbalimbali walioshirikiana nami kuona inafanyika kama ilivyopangwa. Sina budi kutoa shukrani zangu za dhati kwa watu wote walionisaidia katika kufanikisha utafiti huu.

Kwanza, kabisa napenda kumshukuru Mungu kwa kunipa uhai, uzima na afya njema hata nikaweza kufanikisha kazi hii bila matatizo yoyote yale ya kiafya. Pia alinipa akili na ufahamu wa kufanikisha kazi hii na kufikia tamati.

Pili, namshukuru msimamizi wangu, Dkt Muhammed Seif Khatib ambaye amekuwa nami bega kwa bega ili kuhakikisha kazi hii inafikia kiwango hiki. Licha ya yeye kuwa na shughuli nyingi lakini alijitolea muda wake mwingi katika kunisahihisha na kunielekeza pale nilipohitaji msada. Nauthamini sana mchango wake. Mungu ambariki na amzidishie moyo wa imani.

Tatu, naishukuru sana familia yangu akiwemo mke wangu mpenzi Ashura Ali na watoto wetu Nayfat Makame, Ummu Ayman Makame na Suhaila Makame kwa kunikubalia kujiunga na chuo bila kujali upweke walionao na kunisaidia pale nilipohitaji msaada wa hali na mali. Mungu awazidishie baraka na neema katika maisha yao.

Nne, nawashukuru sana rafiki zangu na wanafunzi wenzangu ambao tulishirikiana na kushauriana vyema katika masomo akiwemo Rasuli Muhammed, Haruwa Kheir, Zuhura Said, Arafa Jumanne na Zeyana Omar, kwa pamoja nawatakia kila la kheri katika maisha yao.

Tano, shukurani zangu za dhati kabisa ziwafikie '*Ahlul dhikiri*' wote wakiwemo Makhalifa, Muridi, Watu wazima na Walimu wa Madrasa kwa kunisaidia kupata data mbalimbali za utafiti wangu. Mungu awajaze neema. Mwisho shukurani zangu za pekee kabisa zimfikie mwalimu wangu Dkt. Muhyyidin Ahmad Khamis (maalim Siasa) mkuu wa chuo cha Kiislamu Zanzibar kwa kunisaidia kunipa mwongozo katika utafiti huu. Mungu amzidishie imani na neema katika maisha.

## TABARUKU

Kazi hii ninaitabaruku kwa wazazi wangu Pandu Khamis na Miza Haji kwa kujitolea bila kuchoka ili nisome kadri nitakavyo na kunijengea mazingira mazuri ya kujisomea, kunipa ushauri pale nilipoutaka, kuniamini na kuniombea mema hata nilipokuwa mbali na nyumbani. Pia, tabaruku iwe kwa ndugu zangu wote, Juma Pandu, Yahya Pandu, Haji Pandu na Jina Pandu kwa kuwa nami bega kwa bega pamoja na kuiangalia vyema familia yangu wakati nipo masomoni. Hatua hii ilinitia moyo sana. Mungu awazidishie neema katika maisha yenu nyote.

# IKISIRI

Utafiti huu umehusisha *Chimbuko la Dhikiri: Mabadiliko na Athari zake kwa Jamii ya Wazanzibari*. Chimbuko la tatizo la dhikiri limetokana na uelewa mdogo wa dhikiri, chimbuko lake na sababu ya kuwepo kwa mabadiliko mbalimbali yaliyoikumba dhikiri ya tariqa. Utafiti huu umekuwa na malengo mahsusi matatu ambayo ni kubainisha nini dhikiri, chimbuko na mabadiliko yake. Aidha kubainisha sababu za mabadiliko katika dhikiri na kuchunguza athari zitokanazo na mabadiliko hayo.

Taarifa za utafiti huu zilikusanywa kwa njia ya mahojiano, ushuhudiaji, madodoso na mapitio ya vitabu, makala na majarida. Taarifa hizo zimepatikana kutoka kwa makundi mbalimbali yakiwemo ya walimu wa madrasa, makhalifa, muridi na watu wazima. Uchambuzi wa taarifa za utafiti zilizokusanywa zimeongozwa na nadharia ya *Ubadilikaji taratibu* ambao ulifanyika kwa mbinu ya ufafanuzi. Matokeo ya utafiti huu yameonesha kwamba dhikiri asili yake ni ughaibuni na kwa sasa imekumbwa na mabadiliko kadhaa ambayo huleta athari mbalimbali kwa jamii ya Wazanzibari. Mwisho, utafiti huu umeonesha muhtasari wa utafiti, mapendekezo yake, matokeo ya utafiti yamebainishwa, changamoto za utafiti zimeoneshwa, na mapendekezo kadhaa kwa tafiti zijazo yamependekezwa.

# YALIYOMO

ITHIBATI ........................................ i
IKIRARI NA HAKIMILIKI ........................................ ii
SHUKRANI ........................................ iii
TABARUKU ........................................ iv
IKISIRI ........................................ v
YALIYOMO ........................................ vi

**SURA YA KWANZA : UTANGULIZI KWA JUMLA** ........................................ 1
1.0 Utangulizi ........................................ 1
1.1 Usuli wa Tatizo la Utafiti ........................................ 2
1.1Tamko la Tatizo la Utafiti ........................................ 3
1.2Malengo ya Utafiti ........................................ 4
1.2.1.Lengo la Jumla ........................................ 4
1.2.2 Malengo Mahsusi ........................................ 4
1.3 Maswali ya Utafiti ........................................ 4
1.4 Manufaa ya Utafiti ........................................ 4
1.5 Mawanda ya Utafiti ........................................ 5
1.6 Nadharia ya Utafiti ........................................ 5
1.7 Nadharia ya Ubadilikaji Taratibu ........................................ 5
1.8 Hitimisho ........................................ 6

**SURA YA PILI :MAPITIO YA MAANDIKO MBALI MBALI** ........................................ 7
1.0 Utangulizi ........................................ 7
1.1Maandiko kuhusu Fasihi Simulizi ........................................ 7
1.2 Maisha ya Waasisi wa Dhikiri ........................................ 9
1.2.1 Maisha ya Sayyid Abdul Qadri Jaylani ........................................ 9
1.2.2 Maisha ya Abul Hassan Ali ash Shadhili ........................................ 11
1.3 Dhikiri na Chimbuko lake ........................................ 14
2.4 Maandiko ya Nyimbo za Dini na Kasida ........................................ 18
2.5 Mapengo Yanayojitokeza ........................................ 19
2.6. Hitimisho ........................................ 20

**SURA YA TATU: MBINU NA VIFAA VYA UTAFITI** .................... 21
3.0 Utangulizi .................... 21
3.1Mpango wa Utafiti .................... 21
3.1 Eneo la Utafiti .................... 21
3.2 Walengwa wa Utafiti .................... 22
3.2.1 Jamii ya Watafitiwa .................... 22
3.2.2 Sampuli ya Watafitiwa .................... 23
3.3.0 Ukusanyaji wa Data .................... 24
3.3.1 Vifaa vya Kukusanyia Data .................... 24
3.3.2 Mbinu za Kukusanyia Data .................... 25
3.3.3 Dodoso .................... 25
3.3.4 Mahojiano .................... 25
3.3.5 Ushuhudiaji .................... 25
3.4 Mchakato wa Ukusanyaji wa Data na Udhibiti Wake .................... 26
3.5 Uchambuzi na Uunganishaji wa Data .................... 26
3.6 Uhalali na Uthabiti wa Data .................... 26
3.7 Mpango wa Ripoti ya Utafiti .................... 26
3.8 Vikwazo vya Utafiti .................... 27
3.9 Hitimisho .................... 27

**SURA YA NNE: MJADALA WA MATOKEO YA UTAFITI** .................... 29
4.0 Utangulizi .................... 29
4.1 Chimbuko la Dhikiri Duniani .................... 29
4.2 Mabadiliko katika Dhikiri .................... 47
4.3 Athari za Mabadiliko katika Dhikiri kwa Jamii ya Wazanzibari .................... 57
4.3.1 Athari Hasi za Dhikiri kwa Jamii ya Wazanzibari .................... 57
4.3.2 Athari Chanya za Mabadiliko ya Dhikiri .................... 60
4.4 Hitimisho .................... 60

**SURA YA TANO: HITIMISHO NA MAPENDEKEZO** .................... 62
5.0 Utangulizi .................... 62
5.1 Muhtasari wa Tasnifu .................... 62
5.2 Utoshelevu wa Nadharia .................... 65

5.3 Mchango Mpya wa Utafiti Huu ........................................................................ 66
5.4 Mtokeo ya Utafiti ........................................................................................ 66
5.5 Changamoto za Utafiti ................................................................................ 67
5.6 Mapendekezo .............................................................................................. 68
5.7 Mapendekezo kwa Tafiti Zijazo.................................................................. 70
**MAREJELEO** .................................................................................................. 71
**VIAMBATISHO** ............................................................................................. 74

**Ufafanuzi wa Istilahi Muhimu Zitakazotumika Katika Utafiti Huu**.

**Dhikiri**

Ni moja ya vipera vya fasihi simulizi katika utanzu wa ushairi simulizi lenye maana ya ukumbusho, sala, utajo, dua, kulingania (daawa).

**Tariqa**

Ni neno la Kiarabu lenye maana ya njia au kundi lenye wafuasi.

**Qadiria**

Ni aina ya tawi la dhikiri ambayo huhusisha mkusanyiko wa watu aghlabu katika duara ambao huanza kwa kusoma kasida ambazo hutambwa kwa kucheza na kupiga koo pamoja na ukofi ambao huwa na utaratibu maalumu.

**Shadhilia**

Ni aina ya tawi la dhikiri ambayo huhusisha mkusanyiko wa watu aghlabu katika duara ambao huanza kwa kusoma kasida ambazo hutambwa kwa kucheza bila kupiga kofi ambao huwa na utaratibu maalumu.

**Khalifa**

Ni kiongozi mwongozaji katika dhikiri ambaye hudhikirisha kwa kusoma kasida mbalimbali pamoja na taratibu nyingine. Khalifa anaweza kuongoza taratibu zote za shughuli au akawa anaongoza kughani tu.

**Muridi**

Ni mtu ambaye ndiye kwanza anaingia katika uga wa tariqa na hupewa ijaza na Khalifa kuhusu taratibu na kanuni za ibada hiyo pamoja na mambo ya sharia ya kumtukuza Mwenyezi Mungu.

**Ijaza**

Ni elimu ya awali anayopewa mtu anapoingia katika tariqa na kuchukua ahadi kwa sheikh kufanya yale yanayotakiwa kufanywa katika tariqa.

**Shawishi**

Katika tariqa yupo shawishi ambaye ni mshika bendera, mbali na jukumu hilo huwa ndiye mwitifaki mkuu katika shughuli. Yeye hupewa jukumu la kujua wapi anakaa khalifa, sheikh na wageni wengine katika shughuli.

**Darweshi**

Ni mtu mwenye elimu nyingi ya kisharia ikiwemo elimu ya tariqa.

# SURA YA KWANZA

# UTANGULIZI KWA JUMLA

## 1.0 Utangulizi

Zanzibar ni mjumuisho wa visiwa viwili Unguja na Pemba. Visiwa hivi vina visiwa vyengine vidogo vidogo ambavyo ni; Tumbatu, Uzi, Fundo, Kojani, Kisiwa Panza na Makoongwe. Zanzibar yote imezungukwa na bahari ya Hindi. Kisiwa cha Unguja ni kikubwa, kina urefu wa kilomita 85 na upana kilomita 36, na eneo la kilomita za mraba 1684. Kisiwa cha Pemba ni kidogo kina urefu wa kilomita 67, upana kilomita 22, na eneo la kilomita za mramba 984 (BAKIZA, 2008:41). Watu wa Zanzibar ni wa mchanganyiko wenye asili tofauti, kama ilivyo katika visiwa vingi duniani. Wapo wenye asili ya makabila ya Kibantu, Washirazi, Waarabu na Wahindi.

Uislamu uliingia Zanzibar katika karne ya 10 AD (An-nuur, 1998). Kuingia kwa Uislamu katika visiwa vya Zanzibar kuliwaathiri wakazi na kuwafanya wafate utamaduni huo. Waarabu ndiyo walioipa jina ZANZIBAR kutokana na neno la Kiarabu ZENJ BAR yaani ardhi ya watu weusi. Wazanzibar huzungumza lugha ya Kiswahili yenye chimbuko la Kibantu ikiwa ni lugha yao ya awali na ya asili. Hata hivyo, kuna tofauti ya kilahaja kati ya maeneo ya mikoa ya Zanzibar. Zipo lahaja kuu tatu zilizomo katika visiwa vya Zanzibar ambazo ni; Kimakunduchi na Kitumbatu huzungumzwa Unguja na Kipemba huko Pemba. Katika mkoa wa Mjini Magharibi Unguja makao makuu ya Serekali ya Zanzibar, Kiswahili kinachozungumzwa ni Kiswahili sanifu, kilichosanifishwa mwaka 1930 (Kipacha, 2012: 2-3).

Kwa mujibu wa ofisi ya mtakwimu mkuu ya Serikali ya Zanzibar, sensa ya watu na makazi ya mwaka 2012, Zanzibar ina watu **1, 303, 569** (Afisi ya mtakwimu, 2015),

inaaminika kuwa asilimia 90% ya wakaazi wa Zanzibar ni Waislamu (Sengo, 1992:53). Dhikiri ni ibada ya Waislamu iliyoletwa Zanzibar zamani imekuwa sehemu ya utamaduni na desturi ya watu wa Zanzibar hasa wa vijijini. Dhikiri hiyo hutumia lugha ya Kiswahili na baadhi ya wakati hutumia lugha ya Kiarabu au mseto wa lugha zote.

### 1.1 Usuli wa Tatizo la Utafiti

Kwa karne nyingi sasa tokea kuasisiwa Uislamu katika Bara Arabu na hatimaye kuenea katika mwambao wa Afrika Mashariki, Zanzibar ikiwemo, dhikiri haikuwa dhana ngeni katika fahamu za Waislamu. Hii ni kutokana na asili na chimbuko la dhana hiyo ambayo inaaminika inatokana na maamuru ya Mwenyezi Mungu kupitia kiongozi wa Waislamu, Mtume Muhammad (S A W). Watu wengi katika dunia huishi kwa kufuata imani mbali mbali. Imani hizo zinaweza kuwa za kidini, kimila, kipagani au vinginevyo. Kwa wale wanaoamini dini, hufanya yale yanayoamrishwa na imani ya dini husika. Katika Uislamu kuna mambo kadhaa ambayo kwayo ni sehemu ya ibada na humpasa kila Mwislamu kuyafuata kikamilifu ili kufikia vilivyo katika lengo la kumcha Mungu. Dhikiri ni moja ya ibada katika Uislamu inayoaminika kuwa mtekelezaji hupata fadhila kubwa kutoka kwa Muumba. Utambaji wa dhikiri ni suala linalofanywa na Waislamu wengi takribani duniani kote kwa kuamini kuwa ni lengo la kumtukuza, kumpwekesha, kumlingania na kumuomba Mungu. Jamii ya Wazanzibari kama zilivyo jamii nyingine ambazo watu wake huishi na matatizo mbali mbali ambayo huweza kuathiri maisha ya wanajamii hao. Matatizo hayo kwa kiimani ya dini husababishwa na wanajamii wenyewe kwa kufanya maasi mbalimbali ambayo huaminika kuwa hiyo ni mitihani inayotoka kwa Muumba kwa waja wake kwa lengo la kuwapima upeo wa imani zao. Pamoja na

kuaminika kuwa dhikiri kuwa ni sehemu ya ibada ya kumsifu Mtume, pia dhikiri hutambwa kwa lengo la kuomba maghufira na toba kwa Mungu juu ya makosa mbali mbali ambayo waja wa Mwenyezi Mungu wamekwishayatenda na hivyo huombwa kusamehewa. Hali hii huwafanya waumini wengi kuona kuwa, kutamba dhikiri ndiyo jambo ambalo toba zao zinaweza kufika kwa haraka kwa Muumba, kupokelewa na kupatiwa msamaha muafaka. Aidha, kupitia dhikiri hiyo, waumini hutumia vilio, masikitiko, majonzi na hata kutoa miadi kwa kumuahidi Muumba kuwa hawatarejea tena makosa waliyoyatenda na hivyo hawana budi kusamehewa. Hivyo basi, utafiti huu umeangalia chimbuko, mabadiliko, sababu na athari za dhikiri kwa jamii ya Wazanzibar mwishoni mwa karne ya ishirini hadi sasa. Ibada inayoaminika kuwatakasa waumini. Kipindi hiki ndicho ambacho inaaminika mabadiliko ya dhikiri yametokea kwa Zanzibar.

## 1.1 Tamko la Tatizo la Utafiti

Watafiti na wataalamu mbalimbali wametafiti mambo kadhaa yaliyomo katika jamii kwa lengo la kuangalia matatizo hayo na kuyatafutia suluhisho. Miongoni mwa tafiti hizo ni vipengele kadhaa vya ibada ya kidini vyenye mnasaba na fasihi.

Nawaje (2012:77) alitafiti ili kuthibitisha kuhusu ufasihi wa kasida za madrasa ikiwa sehemu ya fasihi simulizi. Naye, Mwanamosi (2014:31), alichunguza mabadiliko ya kasida dhima na uwasilishaji katika fasihi simulizi. Zipo darzeni kadhaa nyingine za tafiti za kidini zenye mnasaba na fasihi zilizofanywa. Hata hivyo, dhikiri bado haijapewa fursa hiyo ya kutafitiwa hasa katika kipengele cha ufasihi, chimbuko na mabadiliko yake. Hali hii imemsukuma mtafiti kuchunguza chimbuko, mabadiliko, sababu na athari ya dhikiri kwa jamii ya Wazanzibari na kuhusisha na fasihi simulizi katika kipindi cha mwisho wa karne ya ishirini hadi sasa.

### 1.2 Malengo ya Utafiti

#### 1.2.1 Lengo la Jumla

Utafiti huu umelenga kuchunguza chimbuko, mabadiliko, sababu na athari ya dhikiri kwa jamii ya Wazanzibari.

#### 1.2.2 Malengo Mahsusi

a) Kuchunguza chimbuko na mabadiliko yanayojitokeza katika dhikiri ya Zanzibar.

b) Kuchunguza sababu zilizosababisha mabadiliko katika dhikiri ya Zanzibar.

c) Kutathmini athari zitokanazo na mabadiliko ya dhikiri kwa jamii ya Wazanzibari

### 1.3 Maswali ya Utafiti

Utafiti huu umelenga kujibu maswali yafuatayo:

a) Kuna mabadiliko gani yanayojitokeza katika dhikiri ya Zanzibar?

b) Ni sababu zipi zilizopelekea kutokea kwa mabadiliko katika dhikiri ya Zanzibar?

c) Ni kwa kiasi gani mabadiliko ya dhikiri yanaathiri jamii ya Wazanzibari?

### 1.4 Manufaa ya Utafiti

Utafiti huu umeleta manufaa kadhaa wa kadhaa: Mosi, umeamsha urazini wa dhikiri katika jamii kwa kutambua chimbuko na mabadiliko yake. Pili, umeelimisha kuwa dhikiri ikiwa ni kama ibada bado inahusiana na tanzu ya fasihi simulizi kwa vigezo vyake vingi. Tatu, watafiti wameiwezesha jamii kupata maarifa mapya yanayohusu dhikiri. Nne, utafti huu umetoa mwanga kwa tafiti zijazo kutumika yakiwa marejeleo

muhimu na kichocheo kwa tafiti nyingine ili kuendeleza dhikiri katika mfumo wa fasihi simulizi.

### 1.5 Mawanda ya Utafiti

Utafiti huu umefanyika katika Wilaya ya Kaskazini 'A' na Wilaya ya Magharibi Unguja. Utafiti umefafanua kwa kina juu ya chimbuko na mabadiliko yaliyojitokeza katika dhikiri na kubainisha sababu za kutokea kwa mabadiliko hayo sambamba na athari zitokanazo na mabadiliko ya dhikiri kwa jamii ya Wazanzibari.

### 1.6 Nadharia ya Utafiti

Utafiti huu umeongozwa na nadharia ya *Ubadilikaji Taratibu*. Ukusanyaji wa data, uchambuzi na uwasilishaji wake umefanyika kwa kuzingatia misingi ya nadharia hii.

### 1.7 Nadharia ya Ubadilikaji Taratibu

Utafiti huu umetumia nadharia ya *Ubadilikaji Taratibu* (*Evolutionalism*). Nadharia hii ya mawanda ya kibaiolojia hutumiwa pia kwenye uwanja wa fasihi. Wananadharia hii waliitumia kwa kuchunguza Fasihi-simulizi ya Kiafrika na kwa kulinganisha fasihi nyingine. Miongoni mwa wananadharia hao ni Edward Burnet Tylor (1832 -1917) na James George Frazer (1854 - 1941). Wataalamu hawa walilinganisha kazi za Fasihi-simulizi za Kiafrika na zile za Kiulaya na kuziona kuwa zinafanana matokeo yake. Kwa matokeo hayo wakaja na dai kwamba kwa kuwa kazi hizo zinafanana yawezekana sana kuwa jamii zote chimbuko lake latoka katika asili moja.

Dhana ya ubadilikaji taratibu ina misingi yake katika imani kwamba viumbe hai vyote kwa kipindi kirefu vimekuwa katika mchakato wa mabadiliko anuai mpaka kufikia katika maumbo yanayoonekana leo hii. Inaaminika kuwa mabadiliko hayo

yameleta tofauti miongoni mwa binadamu. Wazo linalosimama ni kwamba kuna ukoo mmoja au jamii ambayo imezagaa ulimwenguni pote.Wataalamu hao wanaamini kama itachunguzwa jamii mbili katika kipindi kile kile cha ukuaji wa utamaduni, matokeo yake yataonesha kufanana katika elimu, mila na desturi zao zikiwemo ngano, nyimbo za jadi, miviga, methali, na visakale (Nkwera, 1976:21). Kwa hiyo, wanaubadilikaji taratibu wanaona kwamba ili kuielewa fasihi au utamaduni wa kijadi wa jamii yoyote ile ni bora kulinganisha na nyingine ya aina hiyo toka katika jamii nyingine katika kipindi hicho hicho. Mchango mkubwa wa nadharia hii ni kutambua fasihi-simulizi ya Kiafrika kuwa ipo na haina tofauti kubwa na fasihi simulizi za Kiulaya.

Utafiti huu wa chimbuko la dhikiri, mabadiliko, sababu na athari zake umesadifu sana na utumiaji wa nadharia ya *Ubadilikaji Taratibu* kwani ndiyo hasa inayoshadidia na kuleta mnasaba wa kujenga msingi wa mabadiliko katika fasihi-simulizi na jamii. Nadharia hii imemsaidia mtafiti kueleza, kuchambua na kubainisha chimbuko la dhikiri, mabadiliko, sababu na athari zake ikiwa ni kiini cha utafiti huu.

## 1.8 Hitimisho

Sura hii imeelezea kuhusu usuli wa tatizo la utafiti na kuonesha kwa namna gani mada hii ilivyo na mnasaba na fasihi simulizi katika maisha ya kila siku ya wanajamii. Tamko la utafiti limefafanuliwa kwa kuonesha tatizo lililokuwepo ambalo limemsukuma mtafiti kufanya utafiti huu. Vile vile, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti na mipaka ya utafiti yamefafanuliwa ili kubainisha hali halisi ya utafiti ulivyofanyika. Aidha, nadharia ya *Ubadilikaji Taratibu* ndiyo iliyotumika na imesaidia kwa kiasi kikubwa katika uchambuzi na uchanganuzi wa data za utafiti huu. Sura inayofuata imezungumzia kuhusu mapitio ya maandiko mbali mbali.

# SURA YA PILI

# MAPITIO YA MAANDIKO MBALI MBALI

## 1.0 Utangulizi

Sehemu hii imebainisha maandiko mbalimbali yanayohusiana na mada hii ya utafiti. Maandiko hayo yamegawanywa katika makundi mbalimbali ambayo ni maandiko kuhusu fasihi simulizi, waasisi wa dhikiri za *Qadiria* na *Shadhilia*, dhikiri na chimbuko lake na maandiko ya nyimbo za dini na kasida. Kila kundi limetambulishwa na andiko husika, na mwisho tumeonesha pengo lililojitokeza ambalo limezibwa na matokeo ya utafiti huu.

## 1.1 Maandiko kuhusu Fasihi Simulizi

Wataalamu mbalimbali wa fasihi wamejaribu kutoa mawazo yao juu ya fasihi simulizi na maana yake.

Senkoro (1985:4) amejadili kuhusu dhana ya fasihi simulizi na kuhusisha na hadithi, kuwa ni masimulizi ya kale ambayo hurithishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Mtazamo huu unamaanisha kuwa fasihi simulizi imekuwepo na kutumika tokea zamani hadi sasa na hivi kizazi kilichopo huipokea na kuimarisha. Kwa muktadha huo, fasihi simulizi ni utanzu wa sanaa iliyo hai na ambayo hukua na kubadilika kutokana na mabadiliko ya wakati na mfumo wa jamii husika.

Simiyu (2011:13) naye anaona kuwa fasihi simulizi ni sanaa ambayo nyenzo zake kuu za utunzi ni uwasilishaji, usambazaji wake, ni sauti na vitendo. Na ina sifa ya kutamba, kuwasilishwa kwa matamshi ya mdomo, kuhifadhiwa akilini na kuweza kubadilika kwa mujibu wa muktadha. Huwa na hadhira tendi, ni mali ya jamii, na

uwasilishaji wake hufungamana na utendaji. Fasihi simulizi kwa hivyo kihistoria, ni sanaa kongwe, huzaliwa, hukua au hata kufa isipokuzwa.

Mulokozi (1996:24) amebainisha kuwa fasihi simulizi huundwa akilini na kuwasilishwa kwa hadhira kwa njia ya mdomo. Hivyo basi, fasihi simulizi ni tukio linalotawaliwa na mtambaji, hadhira, fani tendwa, tukio husika, mahali na wakati. Pia huathiriwa na muktadha fulani wa kijamii.

Matteru (1983:27) kwa upande wake anaona kuwa fasihi simulizi ni sanaa itumiayo maneno katika kutoa dhana fulani, na kutegemea sana nyenzo mbalimbali za kuonekana na kusikika zitumiwazo na binaadamu katika kujieleza. Fasihi simulizi kwa mfano hutegemea utendaji ili kukamilishwa misogeo, vitabia na miondoko na vipengele vyengine. Hutumia pia mbinu mbalimbali za sauti ya binaadamu zisizokuwa maneno wala mazungumzo kama vile; miguno, toni, vituo katika sauti, miliolio na kiimbo.

Kirumbi (1975:15) anafafanua kuwa, fasihi simulizi ni masimulizi tunayoyapokea mdomo kwa mdomo.

Wataalamu wote hawa hawakuitaja dhikiri wala hawakuijadili katika tafiti zao. Uchambuzi wa wataalamu hawa hata hivyo unafafanua sifa bainifu tu za fasihi simulizi ambazo zinaoana sana na utambaji wa dhikiri. Kwa mnasaba huu kipera cha fasihi simulizi cha dhikiri inayotumiwa na Waswahili kinaoana sana na tabia za fasihi simulizi. Dhikiri kwa hivyo inakuwa na utambaji, hadhira, tukio, fanani tendwa, mahali na wakati. Ni kipera chenye kutumia miguno, toni, milio na viimbo. Hivyo basi, utafiti wetu unanasibisha na sifa zote za dhikiri kama moja ya vipera vya fasihi simulizi katika utanzu wa ushairi simulizi.

## 1.2 Maisha ya Waasisi wa Dhikiri

Waasisi wakuu wa dhikiri duniani ni Abdul Qadiri Jailani na Abul Hassan Ali Shadhili.

### 1.2.1 Maisha ya Sayyid Abdul Qadri Jaylani

Seyyid Abdul Qadir ni Muajemi. Ni kiongozi mashuhuri. Na ni Sheikh wa Waislamu wa imani yake na ni riwaza njema kwa mawalii na wafuasi wake. Seyyid Abdul Qadir alikuwa Imamu wa Siddikin. Sharafu yake kwa mawalii wenzake anaonekana kama sharafu ya Nabii Muhammad.

Seyyid Abdul Qadir alizaliwa katika kijiji cha Jilan huko Iraq. Alizaliwa usiku wa kuamkia mwezi mosi Ramadhani mwaka 1077 AD. Bi Fatma mama yake, alichukua mimba ya mtoto huyo na hali ya kuwa umri wake ni miaka 60, wakati ambao hapakuwa na tamaa ya kupata mtoto yeyote katika ukoo huu. Siku hiyo Fatma aliyomzaa Seyyid Abdul Qadir inaaminika ilizagaa nuru na ilitapakaa kijiji kizima. Mambo hayakuwa hayo tu, lakini inasemekana hapakuwa na mtu yeyote aliyethubutu kuuangalia uso wake kwa mng'aro na haiba yake. Tabia zake alivyokuwa zasemekana zafanana na zile za Seyyidina Muhammad (S.A.W). Uzuri wake unalinganishwa na ule wa Nabii Yusuf (A.S). Ukweli wake unafananishwa na Seyyidina Abu-Bakar (R.A). Haki yake ni kama ile ya Seyyidina Omar (R.A), na upole wake unashabihiana na wa Seyyidina Othman. (R.A).

Seyyid Abdul Qadir akikua na akiishi katika hali nzuri. Mji wao uliingia neema kubwa kabisa baada ya kuzaliwa kwake. Ishara zilizoonesha kama yeye ni walii ni nyingi zikiwemo; kutamka maneno siku ya mwanzo alipopelekwa chuoni kusoma

Qur an. Maneno yenyewe ni haya; *"Mfanyieni nafasi ya kukaa walii wa Mwenyezi Mungu"*. Kusifiwa kwake na "Abdul" kwa kusema: *"Mtoto huyu atakuwa na mambo matukufu atakayosifiwa mwishoni kwake"*. Ishara ya Mtume aliyompa Baba yake usingizini - kwamba; "*utamzaa mtoto ambaye atakuwa na mambo matukufu atakayosifiwa mwishoni kwake"*. (**Chanzo**: Mtandaoni, ww2.al-faqeer. com, Mei, 2016).

**Kutafuta Elimu**

Seyyid Abdul Qadir alipotimia miaka 18, alimwomba ruhusa mama yake kusafiri kwa kutafuta elimu ambayo kwa Waislamu ni wajibu kwa mwanamke na mwanamume. Aliondoka kwenda Baghdad pamoja na Nabii Khidhri. Seyyid Abdul Qadir alipokuwa Baghdad alifanya ibada kwa miaka mitatu. Seyyid Abdul Qadir alisoma kwa juhudi na ari kubwa na aliwashinda wenzake wote kwa elimu na ufasaha wa lugha. Alikuwa bingwa mkubwa wa madhehebu ya Shafi na Hambali. Akiulizwa hujibu hoja kwa madhehebu hayo mawili. Ingawa yeye mwenyewe alikuwa akifuata Madhehebu ya Hambal. Baadhi ya elimu alizosoma ni *Qur an (Tafsiri), Fiqh, Hadithi, Usuli-fiqh, Tarikh (historia), Tasawuf* na *Lugha*.

**Karama za Seyyid Abdul Qadir**

Karama ni mambo ya ajabu yenye kuthibiti kwa mawalii. Ama mambo kama hayo yanapotokea kwa mitume, huitwa "*miujiza"*. Kwa hakika Seyyid Abdul Qadir alikuwa na karama nyingi mno. Karama zilikuwa ni dalili za kuonesha kama alikuwa ni walii. Baadhi ya karama zake ni pamoja na kwenda mbinguni, kuwasalisha mawalii hewani, kumbusu Mtume mkono wake na kukutana na Mtume kwenye mimbari. Nyingine ni kufuturu nyumba 70, kumfufua maiti aliyekwisha kuoza na

kusilimu kafiri kwa kuona karama za seyyid Abdul Qadir. Miujiza mingine ni mtoto wa kike kugeuka mwanaume na tajiri kuwaona ngamia wake waliopotea. (**Chanzo**: Mtandaoni, ww2.al-faqeer. com, Mei, 2016).

**Kifo cha Seyyid Abdul Qadir**

Seyyid Abdul Qadir alikufa siku ya Ijumaa, Mfungo saba, mwaka 1166 AD. Alizikwa kwenye chuo chake “Babuluzji”. Kafa na umri wa miaka 91. Watu wengi walimiminika mazikoni kwake. Seyyid Abdul Qadir maiti yake ilisalishwa na mwanawe Sheikh Abdul Wahab na alisaliwa na watu wengi wakiwemo; watoto wake, wanafunzi wake na marafiki zake. Sheikh Seyyid Abdul Qadir Jailani ni kiongzi na ni mtu muhimu katika dhikiri ya Qadiria kwani alisimama kidete kuhakikisha dhikiri hii inapata mashiko kwa kuwa na wafuasi wengi zaidi duniani.

### 1.2.2 Maisha ya Abul Hassan Ali ash Shadhili

Abal Hassan alizaliwa Ghumara huko Magharibi ya Morocco mwaka 1196 AD. Jina lake kamili anaitwa Ali Ibn Abdallah Ibn Abal Hassan Shadhili. Imam Abul Hassan alikuwa ni mfuwasi wa *Ahlul Sunnah wal Jamaa* akifuata msimamo wa Sheikh Abal Hassan Al-Asha'ari/shaira, Madh-habu ya Imam Maliki. Inasemekana kuwa kuja kwa sheikh Sayyid Abul Hassan As-Shadhily kulipelekea kukua kwa **Twariqatul Shadhiliyah** na kuenea sehemu nyingine.Tukio la sheikh kuamua kuhamia nchini Masri, kuliifanya *Madrasatul Shadhiliya* kuenea pembe zote za Afrika ya Kaskazini hususan nchi za Misri, Morocco, Algeria na Tunisia. (**Chanzo**: Mtandaoni, ww2.al-faqeer.com, Mei, 2016).

**Karama za Abul Hassan Ali Shadhili**

Sheikh Abul Hassan alijaaliwa karama nyingi. Miongoni mwa hizo ni kuwa, baina ya magharibi na ishaa alimwagiza mwanawe aitwaye Muhammad ampe maji toka katika kisima kilichokuwa hapo *Humaithira*. Naye Muhammad akamueleza baba yake kuwa hayo maji ni maji ya chumvi ila maji waliyonayo ni maji safi na hayana chumvi. Sheikh akaendelea kumuamuru mwanawe ampe maji toka katika kisima kile kilichopo hapo Humaithira. Akapewa nusu akatia mdomoni na nusu akanawa uso. Yale maji aliyokuwa nayo mdomoni akayarejesha katika chombo kile cha kutekea maji na kumwamuru ayarejeshe katika kisima. Alipoyarejesha yale maji ghafla yakawa ni mengi na si maji ya chumvi tena ikawa kwa *idhini ya Allah*. (**Chanzo**: Mtandaoni, ww2.al-faqeer.com, Mei 10, 2016).

Wakati fulani inasemekana sheikh Abul Hassan alikuwa akimsomesha Quran mmoja wa watoto yatima ambaye baba yake alikuwa amefariki na mama yake ni mmoja kati ya wakaazi zawiyani. Ilipofikia msimu wa Hajj, Sheikh aliwaamuru watu wote wafuatane naye, wake kwa waume na watoto. Yule kijana yatima alionesha hamu kubwa ya kufuatana na msafara wa sheikh, mama wa yule kijana akamwomba Sheikh awe chini ya usimamizi wake. Sheikh akamjibu kwa *idhini ya Allah* usimamizi wake utakuwa mwisho wake Humaythira. Hakuna aliyekuwa ameelewa kauli hii ya sheikh. Yule kijana kabla ya kufika Humaithira alipatwa na homa kali na kufariki. Muridi wa sheikh walitaka kumzika pale, lakini Sheikh akawaambia wende naye mpaka Humaithira. Walipofika Humaithira walimkafini na sheikh aliongoza *salat Janaiza* na kumzika na akawa mtu wa kwanza kuzikwa hapo Humaithira.

Abul Hassan alianza harakati za kutafuta elimu akisafiri kuelekea Baghdadi mji ambao ndiyo ulikuwa ukisifika kwa elimu na maarifa mengi. Hapo mji mkuu wa

Baghdad (Iraq) aliambiwa na kushauriwa na mmoja katika masheikh wakubwa Sheikh Abu Al-Fath Al-Waswit kuwa arudi Morocco. Kwa mujibu wa maelezo ya Ibn Sabbagh anasema kuwa alikuwa ni mtu makini na mwenye kufuata *Quran na Sunnah*.

Katika uhai wake sheikh alikuwa akisema kuwa "*Wanafunzi wangu ndio vitabu vyangu*". Sheikh hapa akimaanisha kuwa katika wanafunzi wake wengi ndio wataendeleza Twariqa hii tukufu kwa maandishi ya karama za kiucha Mungu. Miongoni mwa wanafunzi wake ni Abu Muhammad Abdallah Ibn Salama, Madi ibn Sultan, Abu Abdullah al Lihyani na Mufti Izzadin Ibn Abdal Salaam (Muhadith). Mwana Arifat al Khair au Wajihiyah huyu alikuwa binti wa Sheikh na alikuwa na elimu nyingi ikiwemo kuhifadhi Quraan kwa *Qiraa saba* na alikuwa akifundisha wanawake na wanaume makundi kwa makundi. Alijaaliwa ufahamu mkubwa wa elimu ya *Tafsiri ya Quraan*. Muridi wa mwanzo wa Sidi Abal Hassan ambaye alikuja kuendeleza Twariqa katika ni Sidi Abul Abbas Al Mursi aliyezaliwa Mursia nchini Spain (Andalusia). Inaaminika kuwa alikuwa Khalifa wa kwanza baada ya kifo cha Sidi Abal Hassan As-Shadhili

**Wasia wa Sheikh Abul Hassan kwa Wanafunzi wake**

Jioni kabla ya kifo chake aliwaita wanafunzi wake na kuzungumza nao mmoja mmoja na baadae akawaita wote katika Majlisi na kuanza kuwapa wasia wa mwisho. Aliwaambia kila Muridi adumishe kusoma *Hizbu Bahr*, kwani hakika katika *Hizbu Bahr* kuna jina tukufu la Allah (Ismu-Allah Al-Adhwam). Kisha akahusia kwa msisitizo kwa kuwaambia "*wafundisheni watoto wenu*"! Baada ya hapo akaongea na Abul Abbas al Mursi kwa faragha na kumwachia wasia mwingi kumwombea Mungu

na kumpa baraka. Baadaye akawaambia Muridi kuwa pindi akifa wamfate na kumtii Abul Abbas al Mursi kwani yeye ndiye mrithi wake na msimamizi baada yake.

**Kifo cha Abal Hassan Ali Ash Shadhili**

Abal Hassan As-Shadhili alifariki mwaka 1258 AD, akiwa njiani kuelekea kwenye moja ya safari zake za Hijjah na amezikwa Humaithara nchini Misri. Usiku mmoja alipokuwa hai alikuwa katika ibada zake na dhikr na hapo ndipo yalipompata mauti yake. Asubuhi ilipofika muridi wake walimkuta Sheikh ameshafariki na hapo ndipo wakafanya maamuzi ya kumzika hapo Humaithara. *Salat al janaiza* iliongozwa na Sidi Abul Abbas Al-Mursi kisha wakaendelea na safari yao ya Hajj.

Tumeelezea wasifu wao kwa sababu huwezi kuelezea tariqa za *Qadiria* na *Shadhilia* bila kuwahusisha waasisi wake hao ambao ni Abdul Qadir Jailani na sheikh Abal Hassan Ali Ash Shadhili. Pia, masheikh hawa ni wafuasi wa Sufi na waendelezaji wa shule hii ya mawazo. Hii ni kusema kuwa elimu ya tasawuf ina mafungamano makubwa na ibada ya dhikiri. Dhikiri ikipata nafasi ya kuenea katika sehemu kubwa ya ulimwenguni kwa miaka kadhaa.

**1.3 Dhikiri na Chimbuko lake**

Neno dhikiri ni tamko la Kiarabu lenye maana ya ukumbusho, swala, utajo, dua, kulingania (daawa). Pia, neno dhikiri lina maana ya kumtaja Mwenyezi Mungu kwa kumpwekesha na kumtukuza. Dhikiri ya tariqa huhusisha mkusanyiko wa watu (duara) ambao huanza kwa kusoma kasida ambazo hutambwa kwa kucheza na kupiga koo pamoja na ukofi. Kwa kawaida dhikiri hii iko tofauti na dhikiri ya tasbihi kwani kwa upande wa tasbihi watu hawapigi makofi wala koo bali husoma nyiradi

mbalimbali (dua tofauti) huku wakiwa wamekaa na baadhi ya wakati husimama (Muhyiddin, 2015).

Chimbuko la dhikiri ni elimu ya tariqa ambayo Nabii Muhammad alimfundisha Sayyidina Ali. Sayyidina Ali alimuomba Mtume amfundishe njia fupi, bora na rahisi ya kumfikia Mwenyezi Mungu kwa unyenyekevu. Alielekezwa Ali kuwa njia bora ni tamko la 'LAA ILAHA ILLA LLAH', lenye maana "hapana *Mola apaswaye kuabudiwa kwa haki isipokuwa Mwenyezi Mungu*". Inaaminika kuwa Ali alifundishwa na Muhammad naye aliwafundisha masheikh mbalimbali wa wakati huo wakiwemo akina; Sheikh Hassanil Basary, Sheikh Daudi Twabiry na wenzake baadaye ilifika kwa Sheikh Abdul Qadir Jailan (1077-1166) (Muhyiddin, 2015). Masheikh kadhaa walitoka katika miji mbalimbali duniani na kila mmoja aliichukua elimu hiyo ya dhikiri na kwenda kuieneza katika maeneo waliyotoka na kuwa na tariqa zao na ndio maana kukawa na tofauti ya makundi haya ya tariqa ulimwenguni.

1. *Dhikiri ya Qadiria* asili yake ni Bagh-dad ambayo ilienezwa na sheikh Abdul Qadri Jailani ambaye kazaliwa 470 na akafa 561H. Matawi mengine ya dhikiri ni dhikiri ya "Ahmad Tijani" asili yake ni Nigeria na tariqa ya "sheikh Awesu" asili yake ni Somalia. Tariqa ya "Nakshabandy" asili yake ni Uingereza. Hivyo ni dhahiri kuwa, dhikiri hasa ile ya tariqa imeenea katika maeneo wanayoishi Waislamu ulimwenguni kote. Neno *tariqah* au *tariqia* linamaanisha njia ambayo kila tawi la imani hii ya usufi (Usufi njia ya kuelekea kwenye kuiingiza imani moyoni) linaitumia ili kumfikia Mola kwa kusaidia kustawisha sifa za kimaadili na kidini walizonazo wanadamu. Kwa kutegemeana na itikadi zao, kuna aina tatu za *tariqah* ambazo kila moja inayo wafuasi wake.

2. Njia kwa ajili ya matendo mema (*tariq-i akhyar*): Hizi ni *tariqah* zinazozingatia matendo ya ibada na uchamungu. Njia kwa ajili ya watu wema (*tariq-i ebrar*): Hizi ni *tariqah* zinazozingatia kuitakasa roho ya mwanadamu kwa kupitia mazoezi ya kiroho na huduma.
3. Njia kwa ajili ya wapenzi (*tariq-i shuttar*): Hizi ni *tariqah* zinazolenga kufikia malengo ya aina moja kwa kupitia upendo.

Kila moja katika aina hizi tatu za *tariqah* zinawakaribisha watu kulingana na wasifu wao. Kila mtu anajiunga katika *tariqah* ambayo inaendana na utakaso wake na ukamilifu wa kiroho. Kwa kuwa watu wana tabia tofauti, ni jambo la kawaida kuwa na *tariqah* tofauti. Kuna uhusiano mkubwa wa dhikiri ya tariqa na Uislamu kwani dhikiri ni sehemu ya ibada ambapo waumini hupaswa kuifuata kikamilifu kwa lengo la kujitakasa.

**(i) Usufi**

Chimbuko la dhikiri ya *Qadiria* na *Shadhilia* ni mtazamo wa kidini wa shule ya mawazo ya kisufi. Inasemekana kuwa neno "Sufi" limepatikana kutokana na neno la kigiriki "*sophia*", ambalo linatokana na neno la kiarabu "*tasawwuf*". Kwa namna hiyo hiyo kuna wengine wanaojaribu kuchambua asili ya "Sufi" kutokana mila za kabla ya Uislamu, za Kikiristo na Kiyahudi; na bado kuna wengine wanadai kuwa mwenendo wa kisufi umetokana na mizizi ya dini ya Kihindu.

Kwa jumla, nadharia zote hizi zimeshindwa kutoa uelewa wa kweli juu ya kiini cha usufi. Wanazuoni wa Kiislamu nao wametoa maneno mengi na yenye kushawishi katika kuelezea asili ya neno "*tasawwuf*" kama linavyopatikana katika vyanzo mbalimbali vya Uislamu. Kwa mfano, maoni yametolewa kuwa kulingana na historia

ya asili ya neno "*tasawwuf*" limenyambuliwa kutoka kwenye maneno ya kiarabu "*safa*", "*safwah*" na "*istafa*", ambapo maneno yote yanamaanisha 'utakaso'. Baadhi ya wanazuoni wa Kiislamu wanatoa uhusiano wa kihistoria kati ya neno *"tasawwuf"* na sehemu ya jamii ya Waislamu wa mwanzo, ambayo watu wake walijitolea kufanya matendo ya ibada na uvumilivu wakati wote, watu ambao waliitwa *"ahlu'-suffa"*, yani "watu wa utakaso" (Abu Dawud, 1992:8).

Usufi ni elimu kamili ya kiroho katika Uislamu, ambayo inahusiana na mapambano ya ndani dhidi ya matamanio yote ya asili ya binaadamu ambayo yanamuweka mtu mbali na matendo maovu. Lengo la kuumbwa kwa muumini ni kumfanya awe mtumwa wa nafsi yake. Katika muktadha huu upo uhusiano mkubwa kati ya imani ya Sufi na dhikiri. Ili kutekeleza hayo ndipo wafuasi wanatakiwa kumdhukuru Mungu wengine huamini kimya kimya au kumkumbuka Mungu kwa sauti kwa mtindo wa dhikiri. Kwa sababu hii, jambo la kumdhukuru Mola ni la umuhimu wa kwanza katika mafunzo ya Kisufi.

Katika Sufi kuna kanuni kadhaa ambazo ni muhimu kushikamana nazo hasa kwa wale wanaofuata njia ya "Nakshabandy". Kanuni hizo ni kuwa, wakati wote moyo wa Muumini kuwa katika hali ya dhikiri juu ya Mungu, kuzingatia kiwango cha dhikiri, moyo kugubikwa na dhikiri na kuwa na unyenyekevu wa imani wakati unafanya dhikiri. Wasufi huamini kuwa huwezi kuwa Sufi mkamilifu bila dhikiri. Dhikiri kwa hivyo ni moja ya kanuni muhimu inayomfanya mtu kuwa mwanadamu aliyekomaa kiimani (Hanbal, 1992:14).

## 2.4 Maandiko ya Nyimbo za Dini na Kasida

Wakristo mashairi yao au nyimbo zao kuhusu dini huita nyimbo za dini, lakini Waislamu huziita kasida. Hii ni kutokana na tofauti ya kimtazamo baina ya dini hizo. Kineene wa Muteso (2005) amefanya utafiti juu ya kasida ya *Hamziyya na kasida ya Burudai*. Kasida zote hizo zinazungumzia juu ya utukufu wa kiongozi wa dini ya Kiislamu Mtume Muhammad na uwezo wa Mwenyezi Mungu mmoja juu ya kufanya lile alitakalo bila ya ushawishi kutoka kwa mtu mwingine. Kiasili mtunzi wa kasida hizi maarufu ni El- Busery mmoja ya wafuasi wa imani ya sufi.

Nawaje (2012:77) ambaye nimemtaja mapema amechunguza juu ya ufasihi unaojitokeza katika kasida za madrasa. Amechambua juu ya sifa za kifasihi katika kasida hizo na kubainisha kipengele cha dhamira na fani. Amebainisha kuwa kasida ni sehemu ya fasihi simulizi na ni vitu vinavyofanana.

Mdungi (2011) ni mtunzi wa kasida ziliomo katika vitabu mbalimbali. Katika kitabu chake *Malenga wa Uswahilini*, yamo mashairi ya kasida kama vile; *Nguvu za Mola, Thamani ya Pepo na Safari ya Mahaba- Safari ya Msiba*.Tungo hizo zote zinajikita katika uzuri wa kuwa na tabia njema.

Ntarangwi (2004:67) anaeleza kuwa, Waarabu walikuwa na nyimbo zao za dini (kasida) ambazo zilitungwa kwa mpango maalum wa silabi zilizoishia kwa mapigo sawa ya sauti. Mpangilio huu uliendelezwa katika nyimbo za Kiswahili. Kwa wananchi wa upande wa Zanzibar nao walivutiwa na ufundi huo nao wakatunga kwa mistari iliyoishia na silabi sawa. Kwa vile kasida za Waarabu zilikuwa katika mstari mmoja, ilikuwa vigumu kuandika mstari mmoja.

Mulokozi (1996:70) anafafanua kuhusu kuwa tukuzo za dini ni kasida za kumsifu Mtume Muhammad, nyimbo za Wakristo na nyimbo za ibada za jadi. Nyimbo za aina hii huwa na maudhui yanayooana na mafunzo ya dini zinazohusika na Mungu na ibada, dhambi, mapatilizo na mauti, mitume na viongozi wa dini na mahusiano bora miongoni mwa waumini.

Tumeona wataalamu kadhaa wanazizungumzia nyimbo za kidini na kasida. Wote wanaweka uzito katika imani za kidini na kuhusisha na maudhui yake yanavyotukuza na kutweza. Watafiti hawa wote wamejadili kuhusu dhamira na fani ya nyimbo za dini na kasida hata hivyo hakuna alogusia ibada ya dhikiri yenye mnasaba na kasida katika muktadha huu. Hivyo, utafiti huu umechunguza chimbuko la dhikiri, mabadiliko, sababu na athari za mabadiliko yake kwa jamii ya Wazanzibari. Matokeo ya utafiti huu yameziba pengo na ombwe liliopo.

**2.5 Mapengo Yanayojitokeza**

Tafiti zote hufanywa kwa kawaida kulingana na malengo ya maandiko na hulenga kuziba pengo maalum. Hata hivyo, bado mapengo kadhaa yamebainika. Mosi, tafiti nyingi hazijaangalia wala kugusia dhikri. Pili, hakuna tafiti zilizochunguza chimbuko na mabadiliko yanayojitokeza katika dhikiri. Tatu, hakuna maandiko yaliyotazama sababu na athari za mabadiliko ya dhikiri kwa jamii ya Wazanzibari. Hivyo, utafiti huu unaziba mapengo yaliyojitokeza na kutajirisha fasihi simulizi katika vipera vya utanzu wa nyimbo, kasida na dhikiri ambayo imepata mabadiliko na kuondoka katika uasilia wake.

## 2.6. Hitimisho

Katika sura hii ya pili, mapitio mbalimbali ya maandiko yakiwemo yale ya wanataaluma yamepitiwa. Maandiko kuhusu fasihi simulizi, waasisi wa dhikiri za *Qadiria* na *Shadhilia*, dhikiri na chimbuko lake na maandiko kuhusu nyimbo za dini na kasida yamepitiwa na kufafanuliwa kwa kuhusishwa na mada ya utafiti huu. Sura inayofuata imefafanua mbinu mbalimbali ambazo zimetumiwa na mtafiti katika kupata data mbalimbali za utafiti huu.

## SURA YA TATU

## MBINU NA VIFAA VYA UTAFITI

### 3.0 Utangulizi

Sehemu hii imefafanua kwa kina juu ya mpango wa jumla wa utafiti, eneo la utafiti, walengwa wa utafiti, jamii ya watafitiwa, sampuli ya watafitiwa, mbinu na vifaa vya kukusanyia data, mchakato wa ukusanyaji wa data, uchambuzi na uunganishaji wa data na uhalali na uthabiti wa data.

### 3.1Mpango wa Utafiti

Kothari (2004:31) anaona kuwa mpango wa utafiti ni mahusiano ya kimuundo ambapo utafiti hufanyika, na inahusiana na ramani kwa ukusanyaji, upimaji na ufafanuzi wa data. Hivyo, utafiti huu umetumia vianzio vikuu vifuatavyo vya maktabani na ukusanyaji wa uwandani. Kuhusu ukusanyaji wa data wa maktabani, mtafiti amezuru sehemu mbalimbali za maktaba kwa minajili ya kudurusu nyaraka zenye mnasaba na kazi inayokusudiwa kufanywa. Aidha, ukusanyaji wa data uwandani umefanywa kwa kutumia mbinu za hojaji, dodoso na ushuhudiaji ili kubaini chimbuko la dhikiri, mabadiliko, sababu na athari zake kwa jamii ya Wazanzibari. Data mbalimbali zimekusanywa, kuhakikiwa, kuchambuliwa na zimefafanuliwa kwa kina na kuwafikia wasomaji.

### 3.1 Eneo la Utafiti

Utafiti huu umefanyika Zanzibar katika Wilaya za Kaskazini ‘A’ na Wilaya ya Magharibi Unguja. Mtafiti ameteua maeneo haya kwa kuwa ni maeneo muafaka yaliyosaidia kupatikana kwa data stahiki. Katika Wilaya ya Kaskazini ‘A’ wapo Waislamu wengi ambao hutamba kwa dhikiri ya asilia na kwa Wilaya ya Magharibi

hutamba kwa dhikiri ya kisasa. Aidha, ni maeneo ambayo vipo vikundi mbalimbali vya dhikiri ambapo mtafiti wa kazi hii anaishi eneo la Kaskazini ‘A’ Unguja.

### 3.2 Walengwa wa Utafiti

Walengwa wa utafiti huu wamegawanywa katika makundi mawili ambayo ni jamii ya watafitiwa katika ujumla wake na sampuli iliyoshughulikiwa

#### 3.2.1 Jamii ya Watafitiwa

Ponera, (2010:23) anaeleza kuwa jamii ya watafitiwa ni vitu vyote ambavyo mtafiti anaweza kuvitumia kwa ajili ya kupata data za utafiti wake. Jamii ya watafitiwa huweza kuwa kundi la watu, eneo fulani la kijografia, aina ya miti au aina fulani ya maandiko. Katika utafiti huu jamii iliyolengwa kutoa taarifa ilihusu makundi yafuatayo;

i) Watu wazima watano wenye uelewa wa kutosha wa dhikiri na ambao tuliwaamini wanaweza kutoa taarifa sahihi na toshelevu.

ii) Walimu wa madrasa watano wenye uelewa wa dhikiri na ambao katika madrasa zao utambaji wa dhikiri hufanywa.

iii) Mamuridi wa dhikiri watano ambao wana uelewa mzuri wa dhikiri kwa kuwa ndio waitifaki wakubwa katika dhikiri.

iv) Makhalifa wa dhikiri watano ambao ni wabobevu wa dhikiri hasa kwa kuwa wao ndio wataalamu, waongozaji na wafunzaji wa dhikiri kwa mamuridi.

### 3.2.2 Sampuli ya Watafitiwa

Sampuli ni sehemu ya jamii au vitu fulani vilivyochaguliwa ili kutoa taarifa zitakazokuwa kiwakilishi cha jamii nzima. Usampulishaji huo ni mchakato wa kupata taarifa za kundi kubwa kwa kutafiti sehemu ya kundi hilo. Hivyo, usampulishaji ni mchakato wa kuchagua sampuli au njia ya kukusanya data kwa kuchagua sehemu au idadi ndogo ya wawakilishi kutoka katika kundi kubwa la vitu, maeneo au watu (Kothari, 2004:55).

Mbinu ya sampuli lengwa ndiyo iliyotumika. Ni ya wawakilishi wachache waliotafitiwa badala ya wanajamii wote wa utafiti huu. Mtafiti amewachagua wawakilishi hao kulingana na jinsi walivyokidhi haja na malengo ya utafiti huu. Sampuli hiyo ilichaguliwa kibahatinasibu kutoka katika makundi yenye uelewa wa dhikri, ambapo tulikuwa na watafitiwa 20 yaani watafitiwa 5 kutoka kila kundi lililotafitiwa. Watafitiwa hao walikuwa kama vile, watu wazima 5, walimu wa madrasa 5, mamuridi wa dhikiri 5 na makhalifa wa dhikiri 5. Katika watafitiwa hawa hatukuzingatia jinsia bali tumewahoji kutokana na uelewa wao wa dhikiri. Makundi haya yametoa fursa sawa kwa kila mlengwa kutafitiwa na kutoa taarifa sahihi jambo ambalo limesaidia sana kupatikana data za utafiti huu kwa urahisi kuliko kuhoji kila mtu.

Lifuatalo ni jadweli la Sampuli:

**Jadweli 1: Muundo wa Sampuli**

| Na | Sifa za watafitiwa | Idadi ya watafitiwa |
|---|---|---|
| 1. | Watu wazima | 5 |
| 2. | Walimu wa madrasa | 5 |
| 3. | Muridi wa dhikiri | 5 |
| 4. | Makhalifa wa dhikiri | 5 |
| | **Jumla ya watafitiwa** | **20** |

**Chanzo**: Mtafiti, Mei, 2016

### 3.3 Ukusanyaji wa Data

Sehemu hii imefafanua mbinu na zana mbalimbali za ukusanyaji wa data pamoja na mchakato wa ukusanyaji wa data.

#### 3.3.1 Vifaa vya Kukusanyia Data

Hizi ni zana tofauti ambazo tumezitumia katika kukusanya data. Mtafiti ametumia vifaa kama vile; kinasa sauti, kamera, daftari na kalamu pamoja na kompyuta.

**Kinasa sauti**: Kifaa hiki kimesaidia sana katika uchambuzi wa data kwani sio rahisi kuandika mambo yote. Zana hii ameitumia katika mbinu shirikishi na katika mbinu hojaji wakati wa kukusanya data.

**Kamera**: Ilitumika kupiga picha vielelezo mbalimbali vihusianavyo na utafiti huu.

**Daftari la kuandikia na kalamu**: Limetumika kuandikia taarifa mbali mbali pamoja na data zilizokusanywa.

**Kompyuta:** Kifaa hiki kimesaidia sana kwa kutumika kama kifaa cha kuchapia taarifa, kuhifadhi na kuchambua data.

### 3.3.2 Mbinu za Kukusanyia Data

Utafiti huu umetumia mbinu ya kujaza dodoso, mahojiano na ushuhudiaji.

### 3.3.3 Dodoso

Dodoso ni njia moja wapo ambayo imetumiwa na mtafiti katika kukusanya data. Maswali ya dodoso yalijazwa kwa kuzingatia malengo ya utafiti kulingana na makundi ya watafitiwa ambao walikuwa watu wazima, walimu wa madrasa, Makhalifa na Mamuridi. Watafitiwa walitakiwa kujaza dodoso kwa umakini na kwa usahihi kulingana na anavyoielewa mada ya utafiti. Njia hii imemsaidia sana mtafiti kupata taarifa sahihi zinazohusu mada ya utafiti kutoka kwa watafitiwa

### 3.3.4 Mahojiano

Mtafiti ametumia njia ya hojaji kwa watu wazima, mamuridi, walimu wa madrasa na makhalifa wa dhikiri wasio na uwezo wa kusoma na kuandika. Watafitiwa walishiriki moja kwa moja na kutoa taarifa kwa kadri wanavyoelewa kuhusu mada husika ya utafiti. Mbinu hii ilitumika na kusaidia kupata uthabiti wa taarifa zilizotokana na wadau husika.

### 3.3.5 Ushuhudiaji

Mtafiti ametumia njia ya ushuhudiaji kwa kushiriki katika shughuli mbalimbali ambazo hudhikiriwa kwa minajili ya kugundua chimbuko la dhikiri, mabadiliko, sababu na athari zake kwa jamii ya Wazanzibari. Njia hii ilimsaidia sana mtafiti kupata taarifa sahihi na za uhakika kwani alishiriki moja kwa moja katika shughuli za kudhikiri.

### 3.4 Mchakato wa Ukusanyaji wa Data na Udhibiti Wake

Mtafiti ameomba ruhusa kutoka katika mamlaka zinazohusika na zimemruhusu kukusanya data za uwandani na zile za maktabani. Pia, ameomba ridhaa kwa watu binafsi ili watafitiwe na watu hao walikubali kutafitiwa. Aidha, maadili mengine ya utafiti kama vile utunzaji wa siri za taarifa na ufichwaji wa majina ya watoa data yalizingatiwa kwa mujibu wa matakwa ya watafitiwa.

### 3.5 Uchambuzi na Uunganishaji wa Data

Katika utafiti huu mkabala usio wa kiidadi umetumika katika ukusanyaji na uchambuzi data. Mkabala huu umetumika katika kupata taarifa kutoka maktabani na zile za kutoka uwandani. Uchambuzi wa data za utafiti huu umetumia mbinu ya ufafanuzi na uainishaji wa maudhui yaliyojitokeza katika data zilizokusanywa. Maudhui yalibainishwa na kupangwa katika vikundi kulingana na malengo ya utafiti ili kuruhusu kuonesha matokeo na kufikia hitimisho. Maudhui ya kila lengo yalifafanuliwa kwa kina na kulinganishwa.

### 3.6 Uhalali na Uthabiti wa Data

Uhalali wa utafiti ni hali ya utafiti kuwa na uwezo wa kupima mambo yaliyotakiwa kupimwa au kutafitiwa. Uthabiti ni hali ya utafiti kuweza kutoa matokeo yanayofanana ikiwa utapimwa wakati mwingine. Hivyo, katika utafiti huu taarifa zilizokusanywa ni za kweli na zenye kupimika. Taarifa zilikusanywa na kuchanganuliwa kutokana na malengo ya utafiti huu.

### 3.7 Mpango wa Ripoti ya Utafiti

Ripoti ya utafiti huu ina sura tano. Sura ya Kwanza, inahusu mada ya utafiti, usuli wa tatizo la utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, manufaa ya utafiti na nadharia

teule za utafiti. Sura ya Pili, imezungumzia mapitio ya maandiko. Sura ya Tatu, imejumuisha mbinu, vifaa na zana za utafiti. Vilevile, imezungumzia mpango wa utafiti, eneo la utafiti, walengwa wa utafiti pamoja na zana za kukusanyia data. Sura ya Nne, imeelezea kuhusu uwasilishaji, uchambuzi na mjadala wa matokeo ya utafiti kwa kuzingatia malengo ya utafiti. Sura ya Tano, inahusu hitimisho la jumla la utafiti, mapendekezo ya tafiti zijazo na viambatisho lengwa vya utafiti huu.

## 3.8 Vikwazo vya Utafiti

Mchakato mzima wa utafiti ulikabiliwa na matatizo kadhaa katika hatua zake mbalimbali. Baadhi ya watafitiwa hawakuwa rahisi kutoa taarifa hadi walipoeleweshwa kwa kina na mtafiti kuhusu lengo la utafiti. Kingine ni ukata wa fedha kwani vyanzo vilivyotarajiwa kutoa pesa kwa ajili ya mchakato wa utafiti vilichelewa sana kutoa. Hili liliathiri katika utekelezaji wa hatua mbalimbali kwa wakati. Watafitiwa wengi hawajui asili ya dhikiri na sababu ya mgawanyiko wa shule za mawazo na hivyo mtafi alifanya jitihada kubwa kuunganisha mawazo yaliyokuwa yakitolewa na watafitiwa hao.

## 3.9 Hitimisho

Katika sura hii, mambo mbali mbali yamejadiliwa yakiwemo; eneo la utafiti ambalo ni Wilaya ya kaskazini ‘A’ na Wilaya ya Magharibi ‘A’. Hayo ni maeneo ambayo matafiti ameyatembelea na kupata taarifa zinazohusiana na mada hususan habari za kimaktaba. Mpango wa utafiti ni eneo jingine ambalo limejadiliwa katika sura hii, ambapo utafiti huu umetumia mkabala usio wa kiidadi katika ukusanyaji na uchambuzi wa data. Mbinu hii imeteuliwa kutokana na kuwa mada ya utafiti huu si ya kimahesabu. Walengwa wa utafiti huu wamegawanyika katika makundi mawili

yaani kundi la jamii ya wale wanaotafitiwa na kundi la jamii ya sampuli tuliyoshughulika nayo. Jamii ya watafitiwa ambayo ni, watu wazima, walimu wa madrasa, mamuridi na makhalifa. Vilevile sura hii imejadili kuhusu vifaa na mbinu za ukusanyaji wa data kama vile; kinasa sauti, daftari na kalamu, kompyuta, dodoso, mahojiano na ushuhudiaji pamoja na uchanganuzi wa data ambao umezingatia sana malengo ya matatu ya utafiti huu pamoja na vikwazo vya utafiti.

# SURA YA NNE

# MJADALA WA MATOKEO YA UTAFITI

## 4.0 Utangulizi

Sura hii ya nne inahusu mjadala juu ya matokeo ya utafiti. Mjadala wenyewe umegawanyika katika sehemu nne zinazoakisi maswali yaliyouongoza utafiti huu. Sehemu ya kwanza inajadili chimbuko la dhikiri duniani na dhikiri ilivyoingia Zanzibar. Sehemu ya pili inaonesha mtawanyiko na mabadiliko ya dhikiri. Sehemu ya tatu imebainisha na kuelezea sababu za kutokea mabadiliko katika dhikiri za Zanzibar. Sehemu ya nne imefafanua athari za mabadiliko ya dhikiri kwa jamii ya Wazanzibari.

## 4.1 Chimbuko la Dhikiri Duniani

Inaaminika kuwa, chimbuko la dhikiri ni elimu ya tariqa pale Sayyidina Ali alipomwendea Mtume Muhammad na kumtaka amfundishe njia fupi, bora na rahisi ya kumfikia Mwenyezi Mungu. Mtume Muhammad akamwambia njia bora ni tamko la '*LAA ILAHA ILLA LLAH*' lenye maana; *Hapana Mola apasaye kuabudiwa kwa haki isipokuwa Mwenyezi Mungu*. Hiyo ndiyo ikawa chimbuko la dhikiri kisheria (Muhyiddin, 2016).

Baada ya Sayyidina Ali kufundishwa na Mtume naye aliwafundisha masheikh mbali mbali akiwemo Sheikh Abdul Qadir Jailani ambaye aliitoa kwa Sheikh Uwesu wa Somalia. Naye aliifundisha kwa masheikh wengine akiwemo Sheikh Shauri. Masheikh wote hawa walitoka katika miji mbalimbali duniani na kila mmoja aliichukua elimu hiyo na kwenda kuanzisha kundi lake la aina ya tariqa na ndiyo

maana kukawa na tofauti ya makundi haya ya tariqa ulimwenguni (Muhyiddin, 2016).

Sheikh Muhyyidini anafafanua kuwa, chimbuko la dhikiri kwa jumla ni Madina ambako Mtume aliishi kwa wakati huu na ndiko alikofundishwa na Malaika Jibril kutoka kwa Mwenyezi Mungu. Naye Mtume akawafundisha Masahaba dhikiri hiyo na baadaye ikaenea katika miji mbalimbali kutokana na wale masheikh walioipokea na kuitawanya.

Duniani dhikiri zipo za namna mbalimbali ambazo uwepo wake hutokana na aina na mahali ya pale watu wanapodhikiri kwa mujibu wa upokezi wao kutoka kwa yule kiongozi wa kundi husika. Kuna dhikiri za *Tasbihi*, *Qadiry*, *Shadhily*, *Nakshabandy*, *Indarusy*, *Rifai (maulidi ya homu), Tijania*, *Hamziyya* na *Alawiya*. Vile vile aina hizi za dhikiri zinaweza kutofautiana kati ya Zanzibar na maeneo mengine duniani. [1]

i) **Dhikiri Ilivyoingia Zanzibar**

Wakaazi wa pwani ya mwambao wa Afrika Mashariki walioishi pembezoni mwa Bahari ya Hindi, walifanya biashara na nchi za nje kwa kusafiri kwa msaada wa pepo za msimu. Biashara hizi na ujio wa wageni zilifungua milango na maingiliano ya watu walio na tamaduni mbalimbali. Hata hivyo watu wengine kutoka sehemu mbalimbali duniani walikuja kuishi na hatimaye kuoa na kusababisha kuwepo kwa utamaduni wa Waswahili ulioathiriwa na Uislamu. Mnamo karne ya 19 Zanzibar

[1] Mazungumzo kati ya mtafiti na Sheikh Muhyyidin wa tariqatul Qadiria, mkuu wa chuo cha Kiislamu kilichopo Mazizini, Zanzibar Juni 5, 2016

ikawa kituo maarufu cha biashara na kusadifu kuwa moja kati ya vituo vya kutoa mafunzo ya elimu ya dini ya Kiislamu Afrika ya Mashariki. Moja ya dhehebu la Uislamu liitwalo sufi ilichangia sana kuenea kwa Uislamu Afrika Mashariki na kutoa ushawishi wake mkubwa. Imani hii ikawaunganisha waumini na viongozi wa nchi za Zanzibar, Oman, Hadhramaut na Comoro. Hivi basi ibada ya dhikiri ikaenea hata kufata mkondo wa biashara (Nimtz, 1980).

Inaaminika kuwa Zanzibar ilikuwa ni kituo cha mwanzo cha kutoa wataalamu wa Kiislamu weledi katika Afrika Mashariki ambapo tariqa nayo imechangia kuenea huko. Kuenea kwa tariqa katika sehemu mbalimbali Zanzibar kunatokana na kutumika dhikiri katika sherehe mbalimbali kama vile; kusherehekea uzawa wa Mtume Muhammad, sikukuu ya idi al fitri, idi el hajj, kuwepo kwa ziara, arobaini za wafiwa na maziko. Inaaminika kuwa zaidi ya thuluthi moja ya Watanzania ni Waislamu, na inakisiwa asilimia 70% ya Waislamu hao ni wafuasi wa tariqa (Farsy, 1989).

Inaelezwa kuwa kuingia kwa tariqa Zanzibar kunatokana na jitihada kubwa zilizofanywa na watawala wa wakati huo akiwemo; Sayyid Baraghash ambaye kwa makusudi aliwaita waasisi wa tariqa kuja nchini kueneza ibada hiyo. Pia mbali na kuwaita masheikh hao aliwasaidia maisha yao kiuchumi jambo ambalo lilirahisisha kazi hiyo ya kueneza tariqa nchini (Nimtz, 1971).

ii) **Matawi ya Dhikiri Zanzibar**

Watu wa Zanzibar hudhikiri katika maeneo tofauti mjini na mashamba. Hali hii ni kutokana na masheikh wa tariqa hizo ambao ndio walioweka misingi katika visiwa

hivi. Hata hivyo, watu hudhikiri kupitia katika vikundi mbalimbali ambavyo wana-dhikiri wameviunda katika maeneo yao. Aina za dhikiri ambazo zipo Zanzibar ni; *Qadiry*, *Shadhily*, *Rifai*, *Hamziyya* na *Alawiya*. Dhikiri za *Alawiya* huhusisha dhikiri za *kirama*, *kigumi*, *kijiti* na *hochi*. Ukiacha dhikiri za *Tasbihi* baadhi ya wanazuoni wa Zanzibar zote hizo huziita dhikiri "*saadiya*" yaani dhikiri za kifua.

Ingawa zipo aina nyingi za dhikiri Zanzibar lakini katika kazi yetu hii tumejikita kuangalia zaidi dhikiri za *Tasbihi*, *Qadiria*, *Shadhilia* na *Kirama* kwa kuwa ndizo zenye nguvu zaidi Zanzibar. Kupata nguvu kwa tariqa hizi Zanzibar kunatokana na waasisi wake kuwekeza kwa kuzifundisha na ndiyo maana zimepata wafuasi wengi zaidi. Hata hivyo, utafiti umebaini kuwa majina ya tariqa hizi yanakwenda sambamba na majina ya waanzilishi wake wa asili wawili.

a) **Dhikiri ya Tasbihi**

Dhikiri ya awali kabla ya kutoa matawi ilikuwa inaitwa "*dhikiri ya tasbihi*". Inaaminika kuwa Mtume (S.A.W) Nabii wa Waislamu amewafundisha wafuasi wake maneno ambayo ni aina ya dhikiri yenye kumchumia mja (Muislamu) thawabu na kumfutia madhambi yake. Maneno hayo ni kusema kwa Kiarabu; *Subhaana llah (ametakasika Mwenyezi Mungu), Subhaana llah Wabihamdihi Subhaana llahil Adhim (ametakasika Mwenyezi Mungu amatakasika aliye mtukufu), La ilaaha illa llah (hapana Mola anayepaswa kuabudiwa kwa haki isipokuwa Mwenyezi Mungu), La hawla wala Quwwata illa billa (hakuna mwenye hila wala nguvu isipokuwa Mwenyezi Mungu), Subhaana llaah walhamdu lillaah Wallaah akbar (ametakasika Mwenyezi Mungu ashukuriwe Mwenyezi Mungu na yeye ni mkubwa).*

Dhikiri hii hutawaliwa na khushui na unyenyekevu mkubwa wakati wa kuitekeleza ibada hii ambayo mara nyingi huwa baada ya kumaliza kusali. Dhikiri hii inaaminika ndiyo dhikiri ya awali aliyofundishwa Mtume Muhammad na Malaika Jibril akiwa Madina na kuaminika kuwa imetoka kwa Mwenyezi Mungu.

b) **Dhikiri ya Qadiriyya**

Wapo masheikh kadhaa waliofanya jitihada kuingiza dhikiri ya Qadiria Zanzibar akiwemo, Sheikh Muhyyidin Abu Muhammad Al Qadir ambaye alipewa ijaza na Sheikh Uways bin Muhammad, ambaye aliileta tariqa ya Qadiria Zanzibar kutoka kusini mwa Somalia mnamo mwaka 1884 AD (Chiaki, 2007). Tariqa hii ndiyo yenye idadi kubwa ya zawia hapa Zanzibar ambapo kuna zawia 130. Kituo kikuu cha zawia hizo kipo Welezo, kilomita 6.4 kutoka mjini. Sayyid Omar Qullaten ni kiongozi wa dhikiri hii aliyepata ijaza kutoka kwa sheikh Uways bin Muhammad. Sheikh Qullaten ameshafariki na alizikwa huko Masingini, Zanzibar.



***Picha namba 1: Kaburi la Sayyid Omar Qullaten ambaye ni kiongozi wa dhikiri ya Qadiria liliopo Masingini Zanzibar (Chanzo: Utafiti, Juni17, 2016).***

Viongozi hawa walipata mwongozo kutoka kwa masheikh wao na waliunda mtandao mkubwa ujulikanao kwa jina la *Jumuiya ya Zawiyatul –Qadiriyya Tanzania*. Makao makuu yake yalikuwa Dar es Salam lakini kwa sasa yapo Arusha. Vile vile Jumuiya inayo matawi yake katika nchi mbalimbali ikiwemo; Kenya, Dubai, Congo na Burundi. Kazi kubwa inayoendelea kufanywa na Jumuiya hiyo ni kusambaza vitabu vinavyohusu tariqa katika nchi mbalimbali kupitia zawia. Kuenea kwa tariqa ya Qadiria kunatokana na mchango mkubwa wa mwasisi wake ambaye alieneza kwa kuwafundisha wanafunzi wake elimu za *fiqhi* na *tasawuf* ambazo zina mafungamano makubwa na dhikiri (Chiaki, 2007).

Zanzibar na baadhi ya nchi nyingine duniani ikiwemo Somalia, huko dhikiri ya *Qadiria* hii huanza kwa namna ya kipekee watu wakiwa wamekaa kitako kwa kusoma *Maulidi ya Jailani*, *Manaqibu* pamoja na *Maulidi ya Mtume* na kwa pamoja hujulikana kama nyiradi tangulizi za dhikiri (Muhyiddin, 2016). Baadaye sheikh huanza kwa kusoma aya chache katika kitabu cha Mwenyezi Mungu Qur an na kisha baada ya kumaliza huanza kusoma qasida huku wakiwa wamekaa. Wale Muridi ambao wamehifadhi nyiradi na dhikiri ambazo ndani yake zina mafundisho ya ucha Mungu humfuata kwa kukariri asomayo. Baada ya hapo Muridi wa kwanza aliyekaa kuliani mwa sheikh hurudia kusoma aya chache za Qur-ani na anaposema "*Sadaqallahul-Adhim*" sheikh huanza upya kusoma qasida na wote hushiriki kusoma. Hufanya hivyo hivyo kwa kupokezana kwa walioshiriki kusoma japo aya moja, na hushirikiana hivyo mpaka wote waenee. Wakati wanasoma huwa wanayumbayumba kulia na kushoto kwa kufuata sauti ya nyiradi hizo na hatimaye sheikh hunyanyuka na muridi nao hunyanyuka na kufanya duara.

Sheikh hukaa kati kati na huanza kudhikiri kwa kusema "*AAH AAH AAH*" akiwa na maana ya *Allah Allah Allah*. Naye sheikh akizunguka kati kati yao hali ya kumwelekea kila mara mmoja miongoni mwao mpaka panakuwa mtikisiko mkubwa unaofuatishwa na kofi ambao hupigwa kwa lengo la kufuatanisha sauti ya nyiradi na zile za muridi wanaoitikia kasida kwa wakati ule ili ziende sambamba. Vile vile hurukaruka baadhi yao huku na huku kama wamepatwa na pepo au shetani na kupaza sauti za kuimba zilizopangika.

c) **Dhikiri ya Shadhiliyya**

Tariqa hii kiasili ilianzishwa Acra huko Palestine mwaka 1862 AD. Miongoni mwa masheikh waliofanya kazi ya kuileta *Shadhiliyya* Zanzibar ni; Sheikh Al Nurdin Muhammad aliyepewa ijaza na Sheikh Muhammad Ahmad Abu Bakar, ambaye aliileta tariqa hii Zanzibar kutoka Comoro mnamo karne ya 19. Baada ya kupata elimu ya tariqa kutoka nchi za Jeddah na Zanzibar, sheikh Muhammad bin Abu Bakar alirejea Comoro na kukutana na kiongozi wa tariqa ya *Shadhiliya* aitwaye sheikh Abdallah Darwesh. Madhumuni makubwa ya kukutana kwao ilikuwa ni kujadili namna ya kuiendeleza tariqa ya *Shadhiliyya* katika maeneo mbalimbali. Tariqa hii ina jumla ya Zawia sita Zanzibar, ambapo makao makuu yake yapo Dar es Salam na ulimwenguni yapo Lebanon (Fujii, 2007).

Inaaminika kuwa kuja kwa sheikh Sayyid Abul Hassan kulipelekea kukua kwa *Twariqatul Shadhiliyah* na kuenea sehemu nyingine. Tukio la sheikh Sayyid Abul Hassan kuamua kuhamia nchini Misri kuliifanya *Madrasatul Shadhiliya* kuenea pambe zote za Afrika ya Kaskazini hususan nchi za Misri, Morocco, Algeria na Tunisia (Chiaki, 2008).

Zipo zawia mbalimbali ambazo zimewekwa kwa lengo la kufufua vipaji vya vijana kwa kuwafundisha elimu mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuwapatia elimu juu ya ibada ya dhikiri. Makundi yote ya tariqa juu ya tofauti zao, lengo lake ni kumtii na kumcha Mwenyezi Mungu.

d) **Dhikiri ya Kirama**

Tariqa ya *Kirama* nayo ni moja ya tariqa maarufu Zanzibar. Tariqa hii iliasisiwa na sheikh Shauri bin Haji Mshirazi. Sheikh Shauri alizaliwa Tumbatu kaskazini mwa kisiwa cha Zanzibar na baadaye alihamia Donge. Sheikh Shauri ameshafariki na amezikwa Donge Pangamaua. Sheikh alianzisha tariqa hii baada ya kupewa ijaza na kiongozi wa Qadiria aliyeitwa Uways bin Muhammad. Ingawa wapo wanaosema kuwa *Kirama* ni moja ya matawi ya Qadiria lakini Abudul Samad Shadhili na wafuasi wake hawakubaliani na kauli hiyo bali wao wanadai kuwa *Kirama* ni tariqa inayojitegemea. Wao wanaamini kuwa upo uhusiano baina ya *Kirama*, *Qadiria* na *Shadhilia* unaotokana na hasa jina la kiongozi wake “Shadhili”. Leo Zanzibar kuna zawia tano za tariqa ya *Kirama* (Chiaki, 2007).



***Picha namba 2: Kaburi la Sheikh Shauri bin Haji Shiraz ambaye ni kiongozi wa dhikiri ya Kirama liliopo Donge Pangamaua Zanzibar (Chanzo: Utafiti, Juni 22, 2016).***

iii) **Uongozi wa Dhikiri**

Katika dhikiri ya *tariqa* huwepo viongozi mbali mbali ambao hufanya kazi kwa mujibu wa cheo kinavyoelekeza. Viongozi hao ni kama vile; *Muridi* ni mtu ambaye ndiyo kwanza anaingia katika uga wa tariqa, na hupewa *ijaza* na *Khalifa* na taratibu na kanuni za ibada hiyo pamoja na mambo ya sharia ya kumjua Mwenyezi Mungu. *Shawishi* kitariqa ni kiongozi na ni mshika bendera ambaye mbali na jukumu hilo huwa ndiye mwitifaki mkuu katika shughuli. Hupaswa kujua utaratibu mzima wa ukaaji katika shughuli husika ya dhikiri. Anapaswa kujua wapi anakaa *Khalifa*, *Sheikh* na wageni wengine waalikwa katika shughuli hiyo. *Khalifa* huyu anakuwa ni mwongozaji katika dhikiri ambaye hudhikirisha kwa kusoma kasida mbalimbali pamoja na taratibu nyingine. *Khalifa* anaweza kuongoza taratibu zote za shughuli au akawa na kazi ya kughani tu. Yupo *Darweshi* kiongozi mkuu, huyu ni mtu mwenye elimu nyingi ya kisharia ikiwemo elimu ya tariqa na mshauri mwelekezi katika ibada ya dhikiri.

iv) **Muktadha wa Dhikiri**

Dhikiri ni sehemu ya ibada, hivyo hutambwa takribani muda wote inapobidi kufanya hivyo. Dhikiri hutambwa wakati wa msiba hasa ikawa aliyekufa alikuwa mfuasi. Vile vile, dhikiri huwepo katika sherehe za maulidi ya kuzaliwa kiongozi wa umma wa Kiislamu Mtume Muhammad hususan mwezi wa mfunguo sita wakati wa kuadhimisha uzawa wake. Katika baadhi ya madrasa wanafunzi hudhikiri kila siku kama sehemu ya kuzidurusu kasida zao za dhikiri. Pia, dhikiri hutekelezwa kupitia ziara. Ziara hizo zikiwemo ziara za kuzuru makaburini, wakati wa kuzika na ziara za siku maalumu zilizowekwa ambazo hufanywa na wanatariqa sehemu mbalimbali mijini na mashamba.

v) **Nafasi ya Wanawake katika Dhikiri**

Katika Uislamu suala la kumcha Mwenyezi Mungu halimbagui mwanamke wala mwanamme kwani wote wana maamuru sawa katika kulifikia lengo hilo la ucha Mungu. Hivyo hivyo kwa upande wa utendekaji wa ibada ya dhikiri, wanawake nao hushiriki katika ibada hiyo lakini kwa mpango maalum. Kunakuwa na utaratibu maalumu ambao wanawake hutengewa sehemu yao maalumu kwa lengo la kutochanganyika na wanaume. Wanawake nao wanavyo vikundi vyao vya dhikiri ambavyo huwa hawachanganyiki na wanaume na huongozwa na taratibu na kanuni zile zile za kitariqa kama vile kuwa na viongozi na namna ya uanzwaji wake. Pia nao hudhikiri kwa kupiga kofi, kungurumiza vifua na huwa hawavai sare maalumu.

vi) **Mitazamo Juu ya Dhikiri**

Ipo mitazamo mitatu tofauti juu ya uhalali, umuhimu na tija ya dhikiri. Baadhi ya wasomi wa Kiislamu wa Zanzibar wanatofautiana juu ya dhikiri na umuhimu wake na kudai kwamba dhikiri ya kitariqa ilikuwepo wakati wa uhai wa Mtume Muhammad. Kwa upande wa wale wanaopinga wao wanaamini kuwa haikuwepo aina hii ya dhikiri wakati wa Mtume Muhammad. Wao wanaona kuwa haya mambo ya kukusanyika pamoja katika dhikri na kuleta "kelele za visomo" hayakuwepo bali yanatokana na dini ya "*Budhism*". Lipo kundi la jengine la tatu la wasomi wenye mtazamo ambao wanaitazama dhikiri kuwa ni kitu kilichokinyume na dini ya Kiislamu. Kwao wao dhikiri ni uzushi (bidaa). Wanaikana dhikiri kwa lugha ya kukejeli. Beti hizi zinabainisha na kuonesha kuwa kwao dhikiri haina maana na kwamba ni sawa na ibada ya "kukohoa" tu.

*Adhukuriye Jalali* ***haruki akikohoa***
*Siyo dini ya Rasuli* *waima imezuliwa*
*Yahitajia suali* *mashekhe kusailiwa*
***Wapi ilikozuliwa*** *ibada ya kukohoa?*

*Nauliza kwa yakini* *ijapo mtachukia*
*Hudhukuriwa manani* *sifa zake kusifiwa*
*Leo mwaliza rohoni* ***kofi*****,** ***shingo kudemuwa***
*Wapi ilikozuliwa* *ibada ya kukohoa?*

*Huwaona na* ***bendera*** *wanawake kuchukua*
***Tasubihi kuburura*** ***nakutikisa maziwa***
*Dini hii ni khasara* *yawaumiza vifua*
*Wapi ilikozuliwa* *ibada ya kukohoa?*

*Mashekhe mnaosoma* *na vitabu kufunua*

*Dhikiri sasa ni* **ngoma** *kadiri itavyokuwa*

***Imesiri kuwa vyama*** *vya* ***pepo****,* ***vyano*** *kupewa*

*Wapi ilikozuliwa ibada ya kukohoa?*

(**Chanzo:** Muhammed, Mei 18, 2016)

Mshairi anabainisha kuwa ibada hii ya kukohoa si dini iliyoletwa na Nabii Muhammad. Mghani anauliza ibada gani ya kukohoa, kudemka shingo na kudengua kofia? Anaendelea kuhoji ibada gani hutumika bendera, kuburuza tasbihi na wanawake kutikisa matiti? Mshairi haoni uhusiano wa dini na kupiga ngoma kama pungo ambayo inohitaji chano.

Wapo wanaoamini kuwa watu kukusanyika kusimama, kudhikiri au kukaa wakawa wanafanya dhikiri kama “makelele” ni jambo la uzushi. Hayo ni mambo yaliyobuniwa baada ya zile karne tatu za kuingia waasisi wa dhikiri. Inadaiwa waanzilishi wote wa dhikiri wamekuja baada ya karne tatu wao wanaitakidi kuwa ni wabora wa watu hata kuliko Maswahaba. Waasisi na wakubwa wa dhikiri hizo miongoni mwao kihistoria ni pamoja na; Abdul Qaadir Jaylani (470 – 561) na Aliy Shadhily (593 – 656). [2]

[2] Mazungumzo kati ya mtafiti na Khalifa Muhammed wa tariqatul Qadiria katika zawia iliyopo Msikiti Ngamia Munduli, Zanzibar Mei 18, 2016

Wapo wasomi wengine wa Kiislamu ambao wanaokubali kuwepo kwa dhikiri ya koo (*iraa*) na wanadai kuwa pamoja na kuwa wakati wa mtume haikuwa imeenea sana kudhikiri kwa namna hiyo lakini yalikuwepo matukio ambayo yalionesha wazi wazi kuwa mtume Muhammad anakubaliana na kitendo cha kudhikiri kwa namna hiyo (Muhammed, 2016).

Inasemekana kuwa, siku moja Mtume Muhammad alikuwa anapita njiani akawakuta watu wapo katika dhikiri. Mmoja wao akamwambia mwenzake "*usifanye kelele Mtume anakuja*". Mtume aliposikia vile akamwambia kuwa amwache mwenzake wala asimkataze kwani huenda akawa yuko katika mdadi kutokana na ibada ya dhikari anazoleta. Kauli hii inadhihirisha wazi kuwa kuna namna mbalimbali za kumdhukuru Mwenyezi Mungu na hutokea kwa anaeleta dhikari hupandwa na mdadi (Muhyiddin, 2016).

vii) **Utendaji wa Sanaa ya Dhikiri**

Dhikiri ni ibada lakini pia imekuwa miongoni mwa fani inayoendeleza na kustawisha utamaduni wa Waswahili miongoni mwa jamii ya Wazanzibari na ni sehemu ya fasihi simulizi kupitia tanzu zake ambayo ipo katika utanzu wa ushairi simulizi. Sanaa ya dhikiri huonekana pale watambaji wanapodhikiri huku wakitumia mdomo kusoma, kuitikia na kukohoa kwa kuonesha ushiriki wa hadhira tendi ambayo hutumia sauti zao kwa kughani. Huonesha ufundi wao katika kughani na kuzipangilia vizuri sauti wakati wa kudhikiri na kuonesha mitindo mbalimbali kwa kutumia miili yao ikiwemo, kuruka na kupishana ndani ya duara. Utendaji huu wa wanadhikiri wakiwa fanani huziteka fikra, mawazo na macho ya hadhira na kuifanya iwe makini ili kupata ujumbe uliokusudiwa katika hali ya usahihi.

viii) **Maudhui ya Ushairi wa Dhikiri**

Maudhui ya ushairi wa dhikiri ni yenye kubadilika kutegemeana na muktadha na tukio ambalo kwa wakati ule linatendeka katika jamii. Kwa mfano, wakati wa msiba, watu hutamba dhikiri kwa hujikita zaidi na maudhui yenye kuwapa pole na kuwausia subra walioondokewa na jamaa zao. Halikadhalika wakati wa sherehe za kuzaliwa Nabii Muhammad, kasida za dhikiri hulenga kumsifu na kuzipambanua sifa stahiki za kiongozi huyo. Hivyo, kwa mantiki hiyo maudhui ya ushairi wa dhikiri hulenga kuwa na mnasaba juu ya jambo ambalo jamii inakabiliana nalo kwa wakati ule. Vilevile maudhui ya ushairi wa dhikiri huelezea visa na matukio yaliyowatokea Mitume na maswahaba katika maisha yao kama sehemu ya historia. Dhamira zote hizo na nyinginezo huwasilishwa kupitia beti kadhaa za kishairi.

Katika ubeti ufuatao mtunzi anafafanua maudhui yenye mnasaba wa kuiusia jamii juu ya suala zima la kuwa na *subira* kwa mambo mbalimbali yanayowatokea.

*Bingwa wa subira    nabii Ayub Mtume*

*Kavumilia maradhi   yalomkutia Mtume*

*Wadudu kumbughudhi   yuko kitandani Mtume*

*Miaka kumi na nane na miezi kadhaa kavumilia Mtume*

**Chanzo**: Kanda ya kaseti zenj fm, Juni 7, 2016

Katika beti hii mshairi anajaribu kuelezea maisha ya Nabii Ayub pale alipopatwa na mtihani wa maradhi na kuugua na akawa kitandani kwa muda wa miaka kumi na nane, huku akitokwa na mafunza jambo ambalo lilipelekea wadudu kubaki katika mwili wake.  Mshairi ana lenga kuifundisha jamii juu ya suala la kuwa na *subira* pale inapotokea mitihani kwa kujua kwamba mitihani hiyo imeletwa na Mungu na ndiye atakayeiondoa.

Katika ubeti ufuatao mshairi wa dhikiri anaelezea namna jamii ilivyozongwa na maasi kiasi cha kuchanganyikiwa na kutojua la kufanya ili kujinasua na mashaka ya ulimwengu.

*Ulosema umati bora      tunateseka siyee*

*Tufanye nini Mola       tufanye nini Mola*

*Na maasi mengi      yameizama dunia*

*Huwa ya huwa      huwa ya huwa*

**Chanzo**: **Chanzo**: Kanda ya kaseti zenj fm, Juni 7, 2016

Mshairi anafafanua kuwa pamoja na Mwenyezi Mungu kuufanya umma huu kuwa umma bora lakini bado unapata mateso makubwa katika maisha ya kila siku. Hivyo, jamii inamshitakia Mungu kwa kumwuliza tufanye nini ili kuondokana na maasi yaliyoenea ulimwengu mzima.

Pia, ubeti huu wa tatu mshairi anaelezea namna maudhui ya dhikiri yanavyoakisi na kwenda sambamba na muktadha kwa kuwapa pole wanajamii waliopatwa na msiba kwa kusema;

*Msiba ulotufika  umeumbwa na Manani*

*Yatupasa kukumbuka  waja tulo duniani*

*Tusije tukaropoka  tukamsahau Manani*

*Kulia kuomboleza  kwamtoa mtu imani*

*Wafiwa nyote poleni*

**Chanzo**: **Chanzo**: Kanda ya kaseti zenj fm, Juni 7, 2016

Mshairi anajaribu kutoa pole kwa kuiusia jamii kuwa na subira na pole kwa yale yalowafika huku wakikumbuka kuwa Mwenyezi Mungu ndiye aliyeumba mauti kwa waja wake. Anafafanua kuwa kulia na kuonesha huzuni hakujakatazwa lakini si vizuri kwa walofika na msiba kulia kwa kuomboleza huku wakiwa wanapiga

makelele, kwani kufanya hivyo kunaweza kumtoa mtu katika imani na kujikuta anakufuru kwa kuingia katika shirki.

Vile vile, maudhui ya ushairi wa dhikiri hubainisha makosa na adhabu za makosa hayo kwa wale wanaokwenda kinyume na maamuru ya Mwenyezi Mungu. Mshairi anafafanua katika ubeti ufuatao kwa kusema;

*Tujiepushe na balaa la* ***dhulma*** *na* ***ushirikina***

*Dhambi za mwenye* ***kusengenya*** *sawa sawa na* ***fitina***

*Halafu Mtume kasema si faradhi wala sunnah*

*Allah huwaaa*

**Chanzo**: Kanda ya kaseti zenj fm, Juni 7, 2016

Katika ubeti huu, mshairi anainasihi jamii juu ya kujiepusha na kufanya makosa ya dhulma, ushirikina, kusengenya na kufitinishana, kwa kuwa kufanya hivyo kunapelekea kubeba mzigo mkubwa wa madhambi na ni jambo baya na ambalo halipo katika miongozo ya dini yao kwani sio faradhi wala sunnah.

Sambamba na hayo, bado maudhui ya ushairi wa dhikiri yanazidi kubainishwa na kufafanuliwa katika ubeti ufuatao kwa nia ya kuifanya jamii lengwa kuelewa kwa kina maudhui hayo kwa kupata ujumbe uliomo katika mashairi hayo. Mshairi anasema;

*Nabi Yunus Mtume Mtume wa Mungu*

*Mola amemwokoa alipomezwa na chewa*

*Baharini alikuwa Allah huwa*

*Marhaba jadal-husain*

**Chanzo**: **Chanzo**: Kanda ya kaseti zenj fm, Juni 7, 2016

Mshairi analenga kuifahamisha jamii juu ya mkasa uliompata Nabii Yunus Mtume wa Mwenyezi Mungu, ambaye alitupwa baharini na hatimaye kuokolewa na chewa. Chewa ambaye alimmeza Nabii Yunus na baadaye kumpeleka mpaka kwenye maji kidogo na ndipo akaweza kuokoka kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu. Hapa mshairi anajaribu kuionesha jamii namna Mitume ilivyopata shida na misukosuko mbalimbali katika kuongoza umati wa nyakati zao lakini walitawaliwa zaidi na *subra na uvumilivu*.

Kama tulivyokwisha kuona katika mifano ya mashairi ya hapo awali, ni dhahiri kuwa maudhui ya ushairi wa dhikiri hulenga kuzungumzia mambo mbalimbali yanayoihusu na kuizunguka jamii kwa lengo la *kuonya, kuasa, kuelimisha* na hata *kukosoa* kama sehemu ya dhima za fasihi simulizi kwa jumla.

**xi) Bendera katika Dhikiri**

Katika dhikiri panakuwepo bendera ambayo kwa kawaida huwa imeandikwa maandishi makubwa ya "*Laailaha illallah Muhammadu Rasulullah*" yenye maana; *Hapana Mola apasaye kuabudiwa kwa haki isipokuwa Mwenyezi Mungu na Muhammadi ni Mjumbe wake*. Aidha, huandikwa baadhi ya aya miongoni mwa aya za Qur-an zenye kutoa ujumbe kwa wanajamii. Bendera ya dhikiri inakuwa na rangi tatu ambazo ni rangi nyeupe, kijani na nyekundu. Kitariqa, rangi hizi za bendera kila moja hubeba maana yake. Kwa mfano; rangi nyeupe huwa na maana ya Mwenyezi Mungu, rangi ya kijani maana yake Mtume Muhammad na rangi nyekundu ina maana ya Sayyid Abdul Qadri Jaylani. Rangi nyeupe ndiyo inayotumika kuandikia maandishi yanayokuwemo katika bendera (Muhyiddin 2016).




***Picha namba 3: Bendera ya dhikiri yenye rangi tatu, nyeupe, kijani na nyekundu ikiwa na maandishi katikati yaliyoandikwa kwa rangi nyeupe (Chanzo: Utafiti, Juni 17, 2016).***

Katika baadhi ya mikusanyiko ya hadhara ya dhikiri huwa kuna bendera zaidi ya moja, hii inatokana na kuwa na makundi yanayoalikwa kuhudhuria katika hadhara ile ambayo nayo huwa na bendera zao jambo ambalo huufanya mkusanyiko kuwa na bendera zaidi ya moja. Anakuwepo mshika bendera ambaye kwa lugha ya kitariqa hujulikana kama *Shawishi*. Huyu kawaida huwa ni kijana miongoni mwa wale muridi. Utafiti umeonesha kuwa sio makundi yote ya dhikiri yanayoshadidia kuwepo bendera wakati wa kudhikiri. Mtafiti ameshuhudia kuna baadhi ya vikundi vya dhikiri hudhikiri bila kuwepo bendera.



Picha namba 4: ***Hadhara ya dhikiri iliyokusanya makundi tofauti ya tariqa wakiwa na bendera zao na kufanya mkusanyiko wenye bendera zaidi ya moja (Chanzo: Utafiti, Juni 19, 2016).***

**4.2 Mabadiliko katika Dhikiri**

Dhana ya mabadiliko ni pana sana ambayo kwa kawaida huhusu kitu au jambo fulani kubadilika kutoka katika hali moja kwenda katika hali nyingine. Mabadiliko yanapotokea kwa kitu ama jambo lolote lile huweza kuboresha au kudhoofisha kitu au jambo husika. Hii ni kwa sababu hakuna kitu kinachobaki na asili yake katika ulimwengu bila kupitiwa na mabadiliko. Mabadiliko ni tabia ya kila kitu au jambo katika ulimwengu. Vivyo hivyo, kwa upande wa fasihi simulizi kupitia vipera vyake dhikiri ikiwemo nayo imepitiwa na mabadiliko kadha wa kadha ikiwemo utambaji wake. Baadhi ya mabadiliko yake ni kama yafuatayo;

i) **Mavazi katika Utambaji wa Dhikiri**

Suala la mavazi katika utambaji wa dhikiri limekuwa ni eneo moja linaloonesha mabadiliko katika dhikiri. Wanatariqa wa Zanzibar tokea asili wanaeleza kuwa hakukuwa na vazi lililowekwa na wanazuoni kuwa ndilo liwe rasmi na livaliwe katika shughuli mbalimbali za kudhikiri isipokuwa baadhi ya makundi ya kitariqa yalipendelea kuona vazi la kanzu kwa wanaume ndilo livaliwe wakati wa utambaji wa dhikiri. Inafafanuliwa kuwa ilikuwa ni muhimu kwa kila sheikh kuvaa "*kilemba*" na "*juba*" au kuweka "*kishali*" begani ili kuonesha tofauti baina yake na wale muridi. Kulikuwa na namna ya uvaaji wa "*kishali"* hicho kwani kwa anayeweka juu ya bega la mkono wa kulia huonekana kama ni mwenye daraja zaidi na yule anayeweka upande wa bega la mkono wa kushoto huwa ni mtu wa daraja linalofuatia.

Kwa sasa hali hii iko tofauti hasa kwa baadhi ya wafuasi na makundi makubwa ya dhikiri hasa huko ughaibuni huonekana wakitamba dhikiri wakiwa na sare maalumu na wengine na vilemba. Lengo la kuwa na sare hizo ni kuweza kutofautisha baina ya kundi moja la dhikiri na jingine kiufuasi na kuonesha utanashati. Kwa upande wa Zanzibar suala la sare kwa wanadhikiri halijakuwa na nguvu kubwa kwani tumeshuhudia baadhi ya makundi yakiwa na vazi aina moja la kanzu na kilemba kwa sheikh peke yake. Vile vile, wapo ambao huenda katika hadhara za dhikiri wakiwa na mavazi tofauti tofauti yasiyokuwa kanzu na badala yake hushirikiana na muridi wengine kudhikiri bila shuruti yoyote.

Hii ni dhahiri kuwa kwa Zanzibar bado hakujakuwa na vazi maalum kama sare katika hadhara za dhikiri, isipokuwa baadhi ya wafuasi huvaa kanzu zao nyeupe na kofia na vilemba kwa viongozi.

ii) **uundo wa Hadhara ya Dhikiri**

Hadhara ya dhikiri huhusisha mkusanyiko mkubwa zaidi ambao huanza kwa wanadhikiri kusoma nyiradi tangulizi kama ni mwanzo wa kuanza dhikiri. Nyiradi hizo huhusisha*; maulidi ya jailani*, *manaqibu*, *maulidi ya Mtume Muhammad* pamoja na dua ambazo kwa pamoja hujulikana kama *tartibu dhikiri*. Utaratibu huu hufanywa kabla ya kuanza kudhikiri huku watu wakiwa wamekaa na kila muda unavyokwenda ndivyo mdadi wa masheikh na muridi hupanda. Baadaye wote hao huinuka taratibu kwa kuanza kudhikiri. Kama tulivyokwisha dokeza kuwa dhikiri huhusisha mkusanyiko ambao wanatariqa hukaa kwa muundo wa duara lenye wafuasi wengi, lakini hivi karibuni tumeshuhudia muundo mpya wa hadhara ya dhikiri Zanzibar.



***Picha namba 5:* Mtafiti pamoja na *wanadhikiri wakiwa katika duara wamevaa sare katika moja ya sherehe huku wakiwa katika nyiradi kabla ya kuanza mdadi katika zawia ya Msikiti Ngamia Zanzibar***

***(Chanzo: Utafiti, Juni 4, 2016).***

iii) **Dhikiri na Biashara**

*Madrasat Ghulam* iliyopo mtaa wa Mwembe Makumbi Zanzibar, ni moja ya kikundi cha dhikiri chenye chenye maudhui na malengo ya kibiashara, ambacho hudhikiri huku kikiwa na wafuasi wachache takriban tisa ama kumi na siyo mkusanyiko mkubwa kama ilivyozoeleka. Katika uanzwaji wa dhikiri, wao huanza moja kwa moja na kudhikiri na sio kuanza kwa kusoma nyiradi kama inavyoanzwa dhikiri za tokea asili. Wenye shughuli waliolipia hawahitaji kasida itawapotezea muda wao wanataka dhikiri ianze ili wafaidi midenguo na mipasho ya maneno yake. Hali hii inaonesha kwa namna gani mabadiliko yalivyoikumba dhikiri Zanzibar.



***Picha namba 6: Wanadhikiri wa Madrasat Ghulam iliyopo Mwembe Makumbi Zanzibar wakionesha mtindo mpya wa kudhikiri kwa kuwa na idadi ndogo ya wafuasi (Chanzo: Utafiti, Mei 23, 2016).***

iv) **Lugha ya Usomaji wa Kasida za Dhikiri**

Kama tujuwavyo asili ya Uislamu inatokana na kitabu cha Quran kilichoandikwa kwa lugha ya Kiarabu. Kwa upande wa kasida za dhikiri nazo tokea asili husomwa kwa lugha ya Kiarabu kama ndio msingi wake mkuu. Eneo hili nalo limekumbwa na mabadiliko makubwa. Tunashuhudia masheikh walio wengi hivi sasa huzisoma kasida lakini wanatumia lugha ya Kiswahili wanapoongoza tariqa zao. Mabadiliko

katika uga huu wa dhikiri waweza kuwa muafaka kufanya kazi kutokana na ukweli kuwa jamii ya Zanzibar kwa kiasi kikubwa haijui lugha ya Kiarabu. Kutumika lugha ya Kiarabu katika dhikiri ni kuwanyima washiriki haki ya kupata maana kidhima. Mabadiliko haya ya matumizi ya lugha yanaonekana kufanywa kupitia kasida zile zile za zamani ambazo hutafsiriwa kwa Kiswahili au kasida mpya ambazo sasa moja kwa moja hutungwa kwa lugha ya Kiswahili.

v) **Dhikiri ya Vinanda**

Kiasili dhikiri hutambwa huku ikiwa na vionjo mbalimbali ambavyo huifanya ifane, itowe hamasa na shime hasa kwa wale wanaoicheza **ahlul- tariqa**. Vyote hivyo hutokana na mpangilio mzuri wa sauti ya sheikh anapoghani kasida, muridi wanapopaza sauti kwa kuitikia pamoja na ukofi ambao hupigwa kwa kufuatishia sauti ili upatikane mizani na muwala mzuri. Katika hili, utafiti umebaini kuwa, yapo mabadiliko ambayo yamesababishwa na usasa ambayo yameifanya dhikiri ipoteze vionjo vyake.

Tunashuhudia matumizi ya vinanda vipigavyo muziki katika utambaji wa dhikiri kwa baadhi ya vikundi. Badala ya kupiga koo kwa kutumia vifua na kupiga ukofi kwa kutumia mikono sasa imekuwa kinyume chake. Dhikiri hii hutumia tuni zitokanazo na ala za muziki, mfano wa ala hizo ni kinanda na biti. Kutamba kule kwa zamani kwa dhikiri hasa katika kipengele cha sauti ndicho hasa kilichokuwa kinaleta hamasa, msisimko na utamu wa asili katika dhikiri. Mfungamano wa vionjo vya asili vya dhikiri vikiwemo; sauti za kofi, vifua na zile sauti za kughani za muridi wanapoitikia huleta muwala mzuri wa ladha katika hadhara ya dhikiri. Halikadhalika

ushiriki huo unakuwa wa kila mmoja katika dhikiri na siyo kwa wapiga ala wachache tu.

vi) **Vituo vya Mafunzo ya Dhikiri (Zawia)**

Makazi maalumu ambayo vijana wa kitariqa huwekwa na kufundishwa mambo mbalimbali yakiwemo tabia njema, namna ya kumjua Mola wao, kufundishwa elimu za kujitambua na yote yanayofungamana na dhikiri ikiwemo elimu ya sharia huitwa zawia. Tokea zamani vituo hivi vipo na huwa na utaratibu maalum kiuongozi na kiuendeshaji. Kila kituo huwa na kiongozi mkuu ambaye kwa kushirikiana na kamati ya uongozi ya kituo hujadili mambo mbalimbali yanayohusu mwenendo mzima wa uendeshaji.

Vituo hivi vilichukuliwa kuwa ni vyuo muhimu kwa vijana wanaoanza kufundishwa elimu tofauti katika kumjua Mungu na umuhimu wa dhikiri. Kwa wakati huo vituo hivi vilikuwa na vijana wengi ambao walikuwa na shauku ya kujipatia elimu. Hali ilivyo sasa ni tofauti kwani ingawa vituo bado vipo lakini vijana wake ni wachache. Mabadiliko haya makubwa yamesababisha kuporomoka kwa idadi ya wafuasi vijana wanaotimiza ipasavyo ibada hii ya dhikiri. Ni asilimia ndogo ya vijana wanaojiunga na vituo hivyo ukilinganisha na asilimia kubwa ya waliokuwa wakijiunga hapo zamani. Bila shaka hali inakosesha vijana kupata uzoefu na kuwa weledi wa kudhikiri. Aidha vijana wamekosa ibada ya imani yao.

vii) **Kutotekelezwa Ipasavyo Dhikiri**

Dhikiri kama sehemu ya ibada kwa waumini wake haipaswi kuachwa wala kucheleweshwa wakati wake unapofika. Utafiti umebaini kuwa mabadiliko makubwa

yametokea ukilinganisha na zamani. Zamani watu walikuwa wakidhikiri sana bila hata kuzingatia utekelezaji wa ibada nyingine ikiwemo muda wa sala. Yumkini sala zote zilikuwa zinawapita huku wakiendelea kudhikiri. Leo tunashuhudia kuwa kila unapofika muda wa sala, sheikh anayeongoza dhikiri hupiga kofi kwa kuvunja dhikiri na kuwaamuru wanatariqa waende kutekeleza ibada ya sala na hurejea tena kudhikiri baada ya kukamilika zoezi hilo.

## 4.1 Sababu za Mabadiliko katika Dhikiri

Tayari tumeshaona na kujadili kwa kina juu ya mabadiliko mbalimbali yanayoikumba dhikiri ya asili, ambayo yamesababishwa na mambo kadhaa wa kadhaa ya usasa. Baadhi ya mambo hayo ni kama yafuatayo;

i) **Athari za Maendeleo ya Sayansi na Teknolojia**

Moja ya sababu zilizopelekea kuwepo kwa mabadiliko katika dhikiri ni matumizi ya zana za sayansi na teknolojia. Haya ni maendeleo yaliyoiathiri dunia katika nyanja mbalimbali, fasihi simulizi nayo haikusalimika kupitia tanzu na vipera vyake ikiwemo dhikiri. Kipera hiki cha fasihi simulizi kupitia utanzu wa kasida na dhikiiri kimepigwa dafrao na mabadiliko hayo.

Kutamba kwa dhikiri huku na kuhusishwa na tuni za sauti zinazotokana na ala za muziki za kisasa ambazo ni zana za kiteknolojia zimetoa mwelekeo mpya. Kiasili kabla ya ujio wa ala za muziki, dhikiri hutambwa na watu ambao hujikusanya pamoja wakiimba kasida mbalimbali huku zikipambwa na sauti za maumbile ya mwongozaji ambaye sheikh, sauti za waitikiaji muridi, kofi pamoja na sauti zinazotoka vifuani mwa wachezaji koo zao zikiwa kavukavu bila ya kusaidiwa na

sauti za ala za muziki. Mtiririko wa sauti za vijana na wazee, nene na nyembamba, sauti madende na nyororo huinogesha dhikiri. Pia wanapo dhikiri hupaza sauti zao kwa pamoja bila ya msaada wa kipaza sauti.

Mkusanyiko huo kwa ukubwa wake hutosha kuzifungamanisha sauti na kuzifanya zitoke katika hali ya mvuto na mngurumo. Tofauti na ilivyo hivi sasa, kwani tunashuhudia mkusanyiko mdogo kiasi cha kuzifanya sauti zao zisifungamane vyema na hatimaye kusaidiwa na vyombo vya kielektroniki kama vile kinanda na biti. Uhalisia wa dhikiri hupotea pale kanda za dhikiri za CD za sauti au picha hutamka katika shughuli bila wahusika kuwepo.

ii) **Utekelezaji Mdogo wa Tamaduni za Kiislamu**

Uislamu ni mfumo wa maisha wa dini ulioweka utaratibu kwa wafuasi wake kutekeleza ibada. Ibada katika Uislamu ni jambo muhimu sana kwani anayetekeleza ibada hizo ipasavyo hupata thawabu ambazo humpelekea kufutiwa madhambi yake aliyokwishayatenda. Kudhikiri ni miongoni mwa ibada za Kiislamu ambayo inaaminika kuwa anayefanya huwa karibu na Mola wake. Waumini hulifanya hili kwa lengo la kuamini na kutarajia Pepo. Hata hivyo, kwa sasa ni tofauti na zamani kwani imebainika kuwa wapo baadhi ya Waislamu Zanzibar hasa wa mjini wanauona utamaduni wa kudhikiri ni wa kimaeneo na unawahusu watu maalumu. Kwa mfano maeneo mengi ya mashamba watu hudhikiri kuliko mjini, hili huwafanya watu wanaoishi mjini kuona kuwa kudhikiri ni jambo linalowahusu zaidi waishio mashamba. Harakati za maisha ya kimjini yenye vionjo vya tamaduni za kimagharibi na ughali wa maisha huwafanya watu wasiwe na muda wa ibada ya dhikiri. Kwa hali hii dhikiri yaonekana ni ibada ya watu "wasioendelea".

iii) **Tofauti ya Mtazamo wa Dhikiri kwa Wanazuoni wa Wazanzibar**

Ipo tofauti ya mawazo na mtazamo juu ya dhikiri. Suala la hitilafu katika Uislamu ni jambo lisiloepukika hasa ikichukuliwa kuwahi kutokea katika historia mbalimbali za Maswahaba wa Mtume Muhammad na viongozi mbalimbali wa dini. Ipo mifano mingi ya tofauti ya kimitazamo inayoonesha namna viongozi hao walivyokuwa wakihitilafiana mara inapotoka amri ya utekelezaji wa jambo fulani. Hitilafu hizi wakati mwingine ni fursa adhimu ya kujifunza mambo mengi ambayo mtu hajapata kuyajua. Katika dhikiri nako kuna tofauti ya kimitazamo.

Wapo wanaoshikilia mtazamo wa kiyakinifu ambao hudai kuwa dhikiri ni ibada sahihi inayotoka kwa Mwenyezi Mungu kwa waja wake na imekuja kama ibada nyingine kwa lengo la kuwapatia thawabu waja wanaoitekeleza. Vile vile wapo wanaoshikilia mtazamo wa kidhanifu katika suala la uhalali wa dhikiri ambao nao hudai kuwa dhikiri hasa ile ya tariqa ni uzushi uliozushwa na wasomi wa karne zilizopita na hivyo haipaswi kufuatwa. Tofauti hizi za kimitazamo ni moja kati ya sababu zilizopelekea kuwepo na mabadiliko, kwani Waislamu wengine hujiweka pembeni kwa kutanzwa kwani huwa hawajui mtazamo upi ulio sahihi na hatimaye kuifanya dhikiri kuwa na uchache wa wafuasi na sababu kubwa ni kutojua ukweli na undani wa jambo hili.

vi) **Kukosa Muda wa Kujihusisha na Dhikiri**

Mfumo wa maisha katika Uislamu ni changamani na umeweka misingi na njia za utafutaji wa riziki kwa kugawa nyakati za ibada huku ukizingatia maisha halisi ya wanaadamu hasa walio masikini. Zanzibar, Waislamu wamekuwa wakitumia muda mwingi kutafuta riziki na baadhi yao hukosa muda wa kufanya mambo mengine

ikiwemo kudhikiri. Kitabu cha Qur an kinatoa mwongozo wa maisha kwa wanaadamu kwa kusema;

> *"nyakati za mchana ni nyakati za kutafuta maisha na nyakati za usiku ni za mapumziko (nyakati za kufanya ibada kwa wingi)" (Surat Nabai, aya 10-11).*

Ingawa tunaelezwa kupitia kitabu cha Quran kwamba suala la kutafuta riziki na kutekeleza ibada vyote vina umuhimu wa kipekee na lisije likatekelezwa moja na jingine likaachwa kwani ni mambo yanayokwenda sambamba kwa mujibu wa agizo la Mungu. Mwenyezi Mungu amesema; "*Enyi mlioamini mtakaposikia mnada wa sala ya ijumaa kimbilieni kumdhikiri Mwenyezi Mungu na mfunge biashara zenu…na mtakapomaliza kufanya ibada basi tawanyikeni katika ardhi mtafute fadhila…" (Suratul jumaa, aya 9-10).* Ieleweke wazi kuwa aya hii inafafanua kuwa, kutafuta fadhila maana yake ni kutafuta riziki hasa zile za halali, kwa kufanya yote yaani kufanya ibada na kutafuta riziki kwani ibada ipo muda wote.

Ingawa kupitia mwongozo wa aya hizi nidhahiri kuwa jambo la kuleta dhikiri na kutafuta riziki yote yana umuhimu wa kipekee hasa kwa kuwa yamepangiwa muda maalumu lakini kwa mtu masikini wa Zanzibar hayatekelezeki. Mazingira ya hali halisi ya kujitegemea kimaisha ni wakutafuta maisha na si kufanya ibada jambo ambalo limesababisha kupungua kwa muda wa kudhikiri.

v) **Mafungamano ya Dhikiri na Ibada Nyingine**

Utafiti wetu umebaini kuwa uelewa mdogo wa kitaaluma kuhusu fungamano la ibada hizi na namna ya kuzitekeleza ni miongoni mwa sababu zilizosababisha mabadiliko katika dhikiri. Waislamu wengine hasa kwa maeneo ya mashamba

wanaamini kuwa kudhikiri ndiyo pekee kunakoweza kukamilisha suala zima la uchaji mbele ya Mwenyezi Mungu. Aidha, wao wanaona hakuna haja ya kufanya ibada nyingine na kwamba kudhikiri ndiko kunakoweza kukamilisha ibada. Hali hii kwa sasa ni tofaufauti na wakati uliopita ingawa bado wapo wanaoshikilia msimamo ule ule wa kubaki katika kudhikiri hata kama ni muda wa kutekeleza ibada nyingine.

vi) **Dhikiri ni Gharama**

Upo mtindo wa vyama hivi vya dhikiri huwa na sherehe kubwa ya dhikiri ya mwaka katika maeneo tofauti tofauti. Dhikiri hizi huchangiwa chakula na ng'ombe huchinjwa kwa ajili ya karamu. Washabiki wa dhikiri hutoka sehemu mbalimbali kukodi magari na kukesha usiku kucha katika dhikiri. Ibada hii hugharamiwa pesa nyingi kwa watu masikini.

## 4.3 Athari za Mabadiliko katika Dhikiri kwa Jamii ya Wazanzibari

Athari ni neno linalobeba dhana mbili tofauti za *"chanya na hasi"*. Kwa kawaida lizungumzwapo neno athari huwa tunasubiri kujua ni upande gani wa athari hizo zinazotaka kuzungumziwa. Kazi hii imefafanua athari chanya na hasi kama zitakavyojitokeza katika utafiti huu.

### 4.3.1 Athari Hasi za Dhikiri kwa Jamii ya Wazanzibari

Kama tulivyokwisha kueleza kuwa utafiti huu unajadili athari mbalimbali zinazotokana na mabadiliko ya dhikiri katika jamii ya Wazanzibar. Miongoni mwa athari hasi za mabadiliko ya dhikiri ni nyingi zikiwemo;

i) **Kukithiri kwa Maasi Katika Jamii**

Kama tulivyokwisha jadili kuwa yapo mabadiliko kadhaa ambayo yameikumba ibada hii ya dhikiri, mabadiliko ambayo yanapelekea kuwepo kwa athari mbalimbali katika jamii ikiwemo kukithiri kwa maasi. Wapo wanajamii ambao hulichukulia suala la kudhikiri kwa mitazamo finyu kwa kuona kuwa dhikiri si jambo la kiibada, ni la kimaeneo na halipaswi kutekelezwa na kila mtu.

Jamii imekuwa ikiendelea kufanya maasi kadhaa yakiwemo kuiba, kuzini, kutokusali, kudhulumiana, kuoneana, ubakaji na ukatili wa kijinsia. Hata hivyo, kupitia dhikiri, kwa wanaodhikiri huwa ni fursa adhimu kwao ya kukabiliana na Mola wao kwa kumuomba msamaha pamoja na kueleza shida na matatizo yanayowasumbua. Suala la kuacha kumdhikiri Mungu imesababisha kukithiri kwa maasi hayo mengi. Dhikiri iliyodhaniwa ingesaidia sana kuondosha maovu na maasi katika jamii ya Zanzibzr, imeshindwa.

ii) **Kuendelea Kudumu kwa Tofauti za Mitazamo Kiupokezi**

Kwa muda mrefu sasa kumekuwapo na hitilafu miongoni mwa jamii duniani pamoja na Zanzibar juu ya suala la kudhikiri. Makhalifa na Wanazuoni mbalimbali waliipokea dhikiri kutoka kwa Mtume Muhammad waliikubali na kuisambaza kwa kuifundisha lakini kumejitokeza makundi yanayopinga mtazamo wa dhikiri hasa ile ya kitariqa na kusema kuwa dhikiri hiyo ni dhikiri ya kizushi na haipaswi kufuatwa. Tofauti hizi zipo takriban katika pande zote za dunia na Uswahilini. Wanaopinga mtazamo wa "*dhikiri ya kitariqa"* wanadai kuwa Mtume alifundisha "*dhikiri ya tasbihi"* tu na sio *dhikiri ya koo*. Kwa upande wa wanaodai dhikiri ya tariqa inafaa na wao wanatoa hoja kuwa ni namna tu ya kudhikiri. Kwani hata hizo *inshaad* ndizo

zinazosomwa na hata ilipokuwa ikitambwa Mtume Muhammad hakukataza kwa kuwa zipo namna nyingi za kudhikiri. Mtume Muhammad wakati inatekelezwa dhikiri ya koo baadhi ya wakati alikuwa anashuhudia na hakukataza (Muhiyydin, 2016).

Juhudi za makusudi hazijachukuliwa na waumini wa dini ya Kiislamu ikiwemo kutolewa elimu ya kutosha juu ya ukweli wa jambo hili ili kupunguza tofauti ziliopo na na wakati huo huo kutoa hamasa ya utekelezaji wake kwa wanajamii wa Wazanzibari. Kuendelea kudumu kwa tofauti ya kimtazamo na kutopatiwa ufumbuzi wa misimamo hiyo kihoja kumesababisha baadhi ya waumini kubaki njia panda jambo ambalo huathiri mwenendo na ustawi wa ibada ya dhikiri.

iii) **Jamii Kupoteza Lengo la Kudhikiri**

Mbali na malengo ya kuletwa ibada ya dhikiri, baadhi ya waumini wameifanya dhikiri kuwa ni sehemu ya biashara. Ukweli wa dai hili unaonekana dhahiri kwa sasa pale kinapotokea kikundi cha watu wanaotamba dhikiri huku wakisaidiwa na vyombo vya muziki. Si hivyo tu hutamba na kurikodi CD kwa lengo la kuuza na kujipatia kipato. Jambo hili hapo awali halikuwepo. Dhikiri ilitumika kama ni ibada ya Mwenyezi Mungu huku washiriki wake wakiwa na matumaini ya kupata thawabu na kuomba toba kutokana na makosa waliyoyafanya. Jamii ya waumini yaonekana kuathirika na kulipoteza lengo la kuletwa ibada hiyo kutokana na wanaodhikiri na kurikodi CD kwa kuuza kazi hizo kupata pesa tu na sio kupata thawabu. Hata wanaoamua kununua CD hizo kwa kuzisikiliza, hujikuta wanafurahia midundo huku wakijiburudisha na siyo kupata thawabu.

### 4.3.2Athari Chanya za Mabadiliko ya Dhikiri

Athari chanya ambazo zimesababishwa na mabadiliko ya dhikiri katika jamii ya Wazanzibari ni kama zifuatazo;

i) **Dhikiri ni Sehemu ya Mawasiliano Baina ya Mungu na Waja wake**

Ibada ya dhikiri kwa waumini ni moja ya daraja zuri linalowaunganisha waja na Mola wao. Kupitia ibada hii waja huamini kwa hupata fursa ya kuzungumza na Muumba wao juu ya shida mbalimbali zinazowakabili, zikiwemo kumuomba msamaha pale wanapokosea na hata kuomba kuondolewa shida zao za kimaisha na kuongezewa riziki na neema katika maisha yao ya kila siku. Sambamba na hayo, kwa anayedhikiri, huamini chumo bora na kupata thawabu ambazo ni neema kubwa kwa mja akizipata.

Utafiti umebaini kuwa Waislamu wanaopata fursa ya kudhikiri wao huamini kuwa na utamaduni mzuri wenye tija. Wapo wanaoamini kuwa wale waloipa mgongo na kuacha kujihusisha na ibada hii wamekosa thawabu na msamaha wa Mola. Jambo hili limewaathiri na waumini kuzikosa fadhila zitokanazo na ibada hii. Hali hiyo kwa wale wasiodhikiri inawakosesha mawasiliano yaliyofungamanishwa na ibada hii. Vile vile kuwepo kwa mabadiliko katika ibada ya dhikiri kunawaathiri waumini kwa kuwa kutotekeleza ipasavyo ibada ya dhikiri kunawafanya kuwa mbali na Mola wao.

## 4.4 Hitimisho

Katika sura hii, matokeo ya utafiti yamewasilishwa na kuchambuliwa kulingana na maswali ya utafiti. Maswali hayo yameakisi malengo ya utafiti. Mjadala umegawika katika sehemu nne; ya kwanza utafiti umebainisha chimbuko la dhikiri duniani,

ambapo mjadala ulihusisha ufafanuzi wa mambo kadhaa yakiwemo; dhikiri ilivyoingia Zanzibar, Matawi ya dhikiri Zanzibar ambapo mjadala ulihusisha dhikiri za *Tasbihi*, *Qadria*, *Shadhilia* na *Kirama*. Uongozi wa dhikiri, muktadha wa dhikiri, nafasi ya wanawake katika dhikiri, mtazamo juu ya dhikiri, sanaa ya dhikiri, maudhui ya ushairi wa dhikiri na bendera katika dhikiri vimejadiliwa.

Sehemu ya pili imejadili mabadiliko ya dhikiri ambapo mjadala ulihusisha hoja kadhaa kama vile; mavazi katika utambaji wa dhikiri, muundo wa hadhara ya dhikiri, lugha katika usomaji wa kasida za dhikiri, dhikiri kupoteza vionjo vya asili, vituo vya mafunzo ya dhikiri (zawia) na kutotekelezwa ipasavyo dhikiri. Sehemu ya tatu ilihusu sababu mbalimbali zilizopelekea kutokea mabadiliko katika dhikiri ambazo ni pamoja na; athari za maendeleo ya sayansi na teknolojia, utekelezaji mdogo wa tamaduni za Kiislamu, tofauti ya mitazamo ya dhikiri kwa Wanazuoni wa Wazanzibar, kukosa muda wa kujishughulisha na dhikiri pamoja na mafungamano ya dhikiri na ibada nyingine.

Athari chanya na hasi za mabadiliko ya dhikiri kwa jamii ya Wazanzibari zimejadiliwa. Upande wa athari hasi ni pamoja na kukithiri kwa maasi katika jamii, kuendelea kudumu kwa tofauti za mitazamo kiupokezi na jamii kupoteza lengo la kudhikiri. Kwa upande wa athari chanya hoja zilizojadiliwa zinahusisha; dhikiri kuwa ni sehemu ya mawasiliano baina ya Mungu na waja wake. Mjadala katika sura hii ya nne umeongozwa na mkabala wa kinadharia ya *Ubadilikaji Taratibu* ambao kwa kiasi kikubwa umesaidia kupatikana kwa matokeo haya.

## SURA YA TANO

## HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

### 5.0 Utangulizi

Katika sura hii, mtafiti anatoa hitimisho la kazi yote kwa kuelezea mchakato mzima uliopitiwa. Sura hii ina sehemu saba. Sehemu ya kwanza inabeba muhtasari wa tasnifu hii, na ya pili inadokeza kuhusu utoshelevu wa mkabala tulioutumia katika uchambuzi wa data za utafiti huu. Sehemu ya tatu inazungumzia mambo mapya ambayo yameibuliwa na utafiti wetu. Sehemu ya nne inatoa matokeo ya utafiti huu, na sehemu ya tano inajadili changamoto zilizojitokeza wakati wa mchakato wa utafiti wetu. Mapendekezo ya jumla juu ya mambo mbalimbali tuliyoyabaini kuhusiana na utafiti wetu yapo sehemu ya sita na ile ya saba inatoa mapendekezo kwa tafiti zijazo kuhusiana na maeneo yaliyogusiwa na utafiti huu.

### 5.1 Muhtasari wa Tasnifu

Utafiti huu ulijikita kuchunguza chimbuko la dhikiri, mabadiliko na athari zake kwa jamii ya Wazanzibari. Tasnifu hii ina jumla ya sura tano. Sura ya kwanza imeelezea kuhusu usuli wa tatizo la utafiti na kuonesha kwa namna gani mada hii ilivyo na mnasaba na fasihi simulizi hasa kwa kuwa ni fasihi inayoakisi maisha halisi ya kila siku ya wanajamii. Tamko la utafiti limefafanuliwa kwa kuonesha tatizo lililokuwepo ambalo likiwa chimbuko la dhikiri na mabadiliko yake limemsukuma mtafiti kufanya utafiti huu. Vile vile, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti na mipaka ya utafiti yamefafanuliwa ili kubainisha hali halisi ya utafiti ulivyofanyika. Aidha, nadharia ya *Ubadilikaji Taratibu* ndiyo iliyotumika na imemsaidia mtafiti kwa kiasi kikubwa katika uchambuzi na uchanganuzi wa data za utafiti huu.

Katika sura ya pili, mapitio mbalimbali ya maandiko yakiwemo yale ya wanataaluma yamepitiwa. Maandiko kuhusu fasihi simulizi, dhikiri na chimbuko lake na maandiko kuhusu nyimbo za dini na kasida yamepitiwa na kufafanuliwa kwa kuhusishwa na mada ya utafiti huu. Hatimaye maandiko hayo yametumika kubainisha mapengo ya kimaarifa kuhusiana na mada yetu.

Sura ya tatu, imebainisha mambo mbalimbali katika sura hii ambayo yamejadiliwa yakiwemo; eneo la utafiti ambalo ni Wilaya ya kaskazini 'A' na Wilaya ya Magharibi 'A'. Haya ni maeneo ambayo mtafiti ameyatembelea na kupata taarifa zinazohusiana na mada husika. Mpango wa utafiti ni eneo jingine ambalo limejadiliwa katika sura hii, ambapo utafiti huu umetumia mkabala usio wa kiidadi katika ukusanyaji na uchambuzi wa data. Mbinu hii imeteuliwa kutokana na kuwa mada ya utafiti huu si ya kimahesabu.

Walengwa wa utafiti huu wamegawanyika katika makundi mawili, yaani kundi la jamii ya wale wanaotafitiwa na kundi la jamii ya sampuli tuliyoshughulika nayo. Jamii ya watafitiwa ambayo ni watu wazima, walimu wa madrasa, muridi na makhalifa wa dhikiri. Vile vile sura hii imejadili kuhusu vifaa na mbinu za ukusanyaji wa data kama vile; kinasa sauti, daftari na kalamu, kompyuta, dodoso, hojaji na ushuhudiaji pamoja na uchanganuzi wa data ambao umezingatia sana malengo matatu ya utafiti huu, na mwisho ni vikwazo vya utafiti vilivyotokea na jinsi vilivyoshughulikiwa na kutanzuliwa.

Sura ya nne imejadili matokeo ya utafiti ambayo yamewasilishwa na kuchambuliwa kulingana na maswali ya utafiti. Maswali hayo yameakisi malengo ya utafiti. Mjadala umegawanywa katika sehemu nne; ya kwanza imejadili chimbuko la dhikiri duniani ambayo ulihusisha mambo kadhaa yakiwemo; dhikiri jinsi ilivyoingia Zanzibar, matawi ya dhikiri ya Zanzibar ambapo dhikiri za *Tasbihi*, *Qadiria*, *Shadhiliya* na *Kirama* zilijadiliwa.

Vilevile sura hii imejadili muundo wa uongozi wa dhikiri na majukumu yao, miktadha ya dhikiri, nafasi ya mwanamke katika dhikiri na mitazamo juu ya tofauti ya dhikiri. Pia sura imejadili sanaa ya dhikiri, maudhui ya ushairi wa dhikiri na aina na matumizi ya bendera katika dhikiri. Mabadiliko ya dhikiri ambapo mjadala ulihusisha hoja kadhaa zikiwemo za mavazi katika utambaji wa dhikiri, muundo wa hadhara ya dhikiri, lugha ya usomaji wa kasida za dhikiri, dhikiri kupoteza vionjo vya asili, vituo vya mafunzo ya dhikiri (zawia) na kutotekelezwa ipasavyo ibada ya dhikiri. Yote hayo yamejadiliwa katika sehemu ya pili.

Sehemu ya tatu ya sura hii ni  mjadala ambao ulihusu sababu zilizopelekea kutokea mabadiliko katika dhikiri ambazo ni pamoja na athari za maendeleo ya sayansi na teknolojia, utekelezaji mdogo wa tamaduni za Kiislamu, tofauti ya mtazamo wa dhikiri kwa Wazanzibari, kukosa muda wa kujihusisha na dhikiri pamoja na mafungamano ya dhikiri na ibada nyingine. Sehemu ya nne imejadili athari chanya na hasi za mabadiliko ya dhikiri kwa jamii ya Wazanzibari zinabainishwa sehemu ya nne. Athari hasi zinahusisha kukithiri kwa maasi katika jamii, kuendelea kudumu kwa tofauti za mitazamo kiupokezi na jamii kupoteza lengo la kudhikiri. Kwa upande wa athari chanya zilizojadiliwa ni pamoja na dhikiri ni sehemu ya

mawasiliano baina ya Mungu na waja wake. Mjadala katika sura hii ya nne umeongozwa na mkabala wa kinadharia ya *Ubadilikaji Taratibu* ambao umesaidia kupatikana kwa matokeo haya ya utafiti.

Hitimisho la utafiti wetu lipo katika sura ya tano. Sura hii ina sehemu saba. Sehemu ya kwanza imebeba muhtasari wa tasnifu hii, ya pili imedokeza kuhusu utoshelevu wa mkabala tulioutumia katika uchambuzi wa data za utafiti huu, na ya tatu imezungumzia mchango mpya wa utafiti ambao umeibuliwa na utafiti wetu. Sehemu ya nne imetoa matokeo ya utafiti huu, ya tano inajadili changamoto zilizojitokeza wakati wa mchakato wa utafiti wetu, ya sita inatoa mapendekezo juu ya mambo mbalimbali tuliyoyabaini kuhusiana na utafiti wetu, na ile ya saba imetoa mapendekezo kwa tafiti zijazo kuhusiana na maeneo yaliyogusiwa na utafiti huu.

## 5.2 Utoshelevu wa Nadharia

Mkabala tulioutumia katika uchambuzi wa data za utafiti huu ni *Ubadilikaji Taratibu*. Dhana ya ubadilikaji taratibu ina misingi yake katika imani kwamba viumbe hai vyote

kwa kipindi kirefu vimekuwa katika mchakato wa mabadiliko anuai mpaka kufikia katika maumbo yanayoonekana leo hii. Mabadiliko hayo yameleta tofauti miongoni mwa binadamu huku kukiwa na sababu na athari chanya na hasi zisababishazo mabadiliko hayo katika jamii.

Vivyo hivyo, katika fasihi simulizi ya wakati uliopita na  ya hivi sasa kupitia tanzu na vipera vyake ikiwemo dhikiri nayo imekumbwa na mabadiliko kadhaa. Kwa hivyo, wanaubadilikaji taratibu wanaamini kwamba ili kuielewa fasihi na mabadiliko

yake au utamaduni wa kijadi wa jamii yoyote ile ni bora kulinganisha na nyingine ya aina hiyo toka katika jamii nyingine kwa wakati ule ule. Mchango mkubwa wa nadharia hii ni kutambua fasihi-simulizi ya Kiafrika ikiwemo dhikiri kuwa ipo na haina tofauti na fasihi simulizi za Kiulaya ijapokuwa zote zinakumbwa na mabadiliko. Nadharia hii imeakisi sana katika utafiti wetu hasa katika mjadala wa uchambuzi wa data na hatimaye kupata matokeo tarajiwa ya utafiti huu kwa kubainisha chimbuko la dhikiri, mabadiliko, sababu na athari zake kwa jamii ya Wazanzibari.

## 5.3 Mchango Mpya wa Utafiti Huu

Kutokana na utafiti huu yapo mambo ambayo yamebainika kuwa ni mchango mpya katika uwanja wa fasihi simulizi. Zipo tafiti nyingi za kitaaluma zimechunguza mambo kadhaa katika fasihi simulizi, baadhi ya hizo zilijikita kuchunguza mambo ya vipengele yva dini na kasida zikiwemo lakini hakuna tafiti zilizotafiti masuala yanayohusu dhikiri ikihusisha maana, chimbuko na mabadiliko pamoja na athari zake kwa Wazanzibari. Vilevile, utafiti huu umetoa mwanga na mchango mkubwa kwa watafiti wengine wanaojikita kuchunguza mambo mbalimbali katika uga wa fasihi simulizi katika kipengele cha dhikiri. Pia utafiti huu umeongeza uelewa wa dhikiri kwa wanajamii hasa wale wasioifahamu vyema na chimbuko lake ibada hii.

## 5.4 Mtokeo ya Utafiti

Utafiti huu umelenga kuchunguza chimbuko la dhikiri, mabadiliko, sababu na athari zake kwa jamii ya Wazanzibari. Katika kuchunguza hayo utafiti huu umeongozwa na malengo mahsusi matatu. Kwanza**,** kuchunguza maana ya dhikiri, chimbuko na mabadiliko yake. Pili, kuchunguza sababu zilizosababisha mabadiliko ya dhikiri.

Tatu, kutathmini athari zitokanazo na mabadiliko ya dhikiri kwa jamii ya Wazanzibari. Utafiti umefanikiwa kufanikisha malengo yote matatu kikamilifu na kuisaidia jamii kujua maana ya dhikiri, chimbuko na mabadiliko yake ambayo yameikumba dhikiri kwa vipindi mbalimbali.

Pia, utafiti huu umebainisha sababu kadhaa ambazo ndizo zilizopelekea kutokea kwa mabadiliko katika dhikiri, sababu hizo zimepatikana kutoka katika vyanzo vyetu halisi vya utafiti huu baada ya kuwahoji watafitiwa. Sababu hizo zimebainishwa na kufafanuliwa kwa lengo la kuielekeza jamii kuzifahamu vyem na namna ya kuzifanyia kazi.

Aidha, utafiti huu umeonesha na kufafanua athari za mabadiliko katika dhikiri na jinsi yanavyoleta athari kwa wanajamii wa Zanzibar. Athari mbalimbali zikiwemo chanya na hasi zimefafanuliwa kwa namna zinavyoiathiri jamii ya Wazanzibari.

### 5.5 Changamoto za Utafiti

Changamoto zilizojitokeza wakati wa utafiti huu ni pamoja na baadhi ya watafitiwa ambao ni walimu wa madrasa, watu wazima, muridi na makhalifa wa dhikiri walikataa kuhojiwa na mtafiti kutokana na madai ya kutolifahamu lengo la utafiti huu, hivyo mtafiti alilazimika kuwabembeleza kwa kuwaeleza lengo la utafiti huu. Hatimaye walikubali kutoa taarifa za utafiti. Maisha ya umasikini ya watafitiwa yameweza kuathiri utafiti huu kwa sababu baadhi ya watafitiwa walikuwa hawapo tayari kutoa taarifa mpaka walipwe fedha. Hali hii ilimlazimu mtafiti kuwaomba wakuu wa makundi ya dhikiri (makhalifa) kuwashawishi watafitiwa waweze

kukubali kutoa taarifa za utafiti kwa sababu utafiti huu ulikuwa wa kitaaluma na siyo wa kibiashara.

## 5.6 Mapendekezo

Utafiti huu ulilenga kuchunguza mambo yanayohusu dhikiri kwa kubainisha maana, chimbuko lake, mabadiliko, sababu za dhikiri na athari zake kwa jamii ya Wazanzibari. Hata hivyo, mapito na michakato yake mbalimbali ya ukusanyaji wa data na uchambuzi ilibaini udhaifu mkubwa uliomo katika jamii juu ya utekelezaji wa ibada ya dhikiri. Kutokana na matokeo ya utafiti huu, mapendekezo yafuatayo yanaweka bayana kusaidia wafuasi wa ibada ya dhikiri kwa Wazanzibari; Mosi, wanadhikiri wengi hudhikiri kwa mazowea tu, kwani baadhi yao hufanya hivyo bila ya kuwa na taaluma ya ibada hiyo huku wakiwa na imani kuwa wanatimiza jukumu la kiutamaduni tu. Kwa kuwa dhikiri ni jambo la kiibada, ni vyema kwa wanatariqa wote kuisoma elimu ya *tasawuf* kwa upeo mkubwa ili kuielewa kwa undani dhikiri. Kwani, *tasawuf* ina mafungamano makubwa na dhikiri na hapo ndipo tija ya dhikiri huweza kupatikana. Vile vile waumini wakumbuke lengo la ibada hii kila wakati kuwa anayedhikiri anapata thawabu kwa Mwenyezi Mungu.

Pili, asili ya dhikiri hasa ile ya tariqa (dhikiri ya koo) inatokana na vionjo vya koo na ukofi ambavyo hupigwa ili kutoa muwala wa sauti na zile za waitikiaji na siyo vyenginevyo. Hivyo, si vyema kwa jamii kuukumbatia usasa kutokana na mtindo wa kudhikiri unaosaidiwa na ala za muziki kwani watu huacha kupiga koo huku wakibaki kuitikia kasida tu. Dhikiri ni jambo la kiibada katika jamii ya Waislamu hivyo haipaswi kuingizwa vionjo visivyo sitahiki kwani linataratibu zake.

Tatu, tofauti za kimitazamo kuhusu dhikiri baina ya wanajamii, hazina manufaa kwa wafuasi. Ni vizuri kwa wale wanaoifahamu elimu ya tariqa kuwafundisha wengine ili kujua na kubaini ukweli na uhalali wa jambo hili la kudhikiri. Endapo wenye elimu watazitumia ipasavyo elimu hizo kwa kuwafundisha wengine hapana budi jamii itaelewa ukweli huu na hivyo kuondokana na tofauti za mitazamo miongoni mwa wanajamii. Hatimaye jamii kuipenda dhikiri na hivyo kuongeza ufuasi kwa kutenda ibada hii.

Nne, ni jambo jema kuendelea kuwepo kwa vituo vya kutolea mafunzo (zawia) kwa vijana ili kuwalea kiroho kwa kuwapatia elimu ya kumjua Mwenyezi Mungu na kuwa na tabia njema. Katika zawia, vijana hujengwa na kulelewa kiimani pamoja na kufundishwa elimu mbalimbali kuhusu dini yao ikiwemo ibada ya dhikiri. Viongozi wa zawia waitwao *makhalifa* wanao wajibu mkubwa wa kufanya juhudi ya kuwashajiisha vijana kujiunga na kukaa katika *markazi* hizo ili kupata maarifa, kwani kwa sasa zawia hizo zinaonekana kuwa na uchache wa vijana hao kutokana na kukosa mwamko na ushajihishwaji.

Tano, wanajamii ni vyema wakaondoa dhana potofu ya kuamini kuwa ibada ya dhikiri ni jambo la kimaeneo na ibada ya vijijini na mashamba. Hii inatokana na kuwa katika jamii wapo watu wanaodhani kuwa dhikiri ni jambo linalotokana na watu wa eneo fulani. Hii ni ibada inayopaswa kufuatwa na Waislamu wote. Kwa mfano ; kwa Zanzibar wapo wanaoamini kuwa dhikiri inahusu jamii ya Watumbatu kwa kuamini kuwa ndiyo wanaodhikiri sana. Dhikiri bado itabaki kuwa ni ibada inayomuwajibikia kila Mwislamu kuitekeleza kwa nia ya kuomba toba ili kusamehewa makosa na kupata thawabu kwa Mwenyezi Mungu.

## 5.7 Mapendekezo kwa Tafiti Zijazo

Hadi itakapojulikana vinginevyo kutoka katika vyanzo vingine vya kutunzia nyaraka za kitaaluma, mpaka sasa tunaamini kwamba utafiti huu ambao umechunguza maana ya dhikiri, chimbuko lake, mabadiliko, sababu na athari zake kwa jamii ya Wazanzibari, ni wa kwanza. Vilevile, pamoja na kuamini kwamba matokeo ya utafiti wetu umezungukia vema na kwa kina eneo la tatizo la utafiti, tunakiri pia kuwa kuna haja ya tafiti zaidi kufanywa katika maeneo mengine.

Katika utafiti huu kuna mambo kadhaa ambayo yanahitaji tafiti zaidi. Sababu kubwa iliyopelekea hilo ni kwamba utafiti huu haukuweza kuziba mianya yote kutokana na mipaka ya mada ya utafiti wetu. Tunatarajia kwamba maeneo hayo yakitafitiwa zaidi kwa kutumia ama mikabala tofauti na ule wa *Ubadilikaji Taratibu* ambao tumeutumia, yanaweza kutoa matokeo mapya na yaliyo bora zaidi.

Utafiti unaweza kufanywa kwa kuangalia tofauti za kimtazamo na kimuktadha kati ya dhikiri za *Shadhiliya* na *Qadriya*. Vile vile tafiti zaidi zinaweza kufanywa kwa kutazama matumiza ya tamathali za semi katika kuwasilisha maudhui ya ushairi wa dhikiri.  Aidha, utafiti unaweza kufanywa kuchunguza ufasihi katika dhikiri.

# MAREJELEO


Abu Dawud (1992) *Sunanu Abi Dawud*, I-V, Istanbul. Minnesota Press.

Ahmad ibn Hanbal (1992) *Al-Musnad*, I-IV, Istanbul. Minnesota Press.

Al-Mubarakpuri, S. (2004) *Tafsiri ya Ar- Raheeq Al-Makhtum*. Ibin Hazm Media Center, Dar es Salaam.

BAKIZA (2008) *Utamaduni wa Mzanzibar*. Zanzibar Quark Express Printing Services.

________ (2010) *Kamusi la Kiswahili Fasaha*. Oxford University Press, East African Limited.

________ (2012) *Kamusi la Lahaja ya Kipemba*. Oxford University Press, East African Limited.

Chum, H. (1974) *Utenzi wa Nushur (Johari za Kiswahili)*. East African Literature Bureau, Nairobi.

Farsy, A. S. (1989) The Shafi Ulama of East Africa. ca 1830 – 1970: A Hagiographic Account, tr. R.L, Pouwels. Modson: University of Wisconsin African.

Faqih, H. (1980) *Utenzi wa Rasil- Ghul*. Tanzania Publishing House, Dar ea Salaam**.**

Fujii, C. (2007) Data on Zawiyas in Contemporary Zanzibar. Kyoto Bulletin of Islamic Area Studies 1 (1), pp. 135-149.

_______ (2008b) Tariqas without Silsilas: The Case of Zanzibar. Kyoto Bulletin of Islamic Area Studies, 2/1: 23-34.

*Kaynak.islamicpublishing.net*, Juni 21, 2016.

Kipacha, A. (2012) *Launi za Kiswahili Sanifu na Kiswahili Fasaha kwa Tanzania Bara na Zanzibar*. Katika Swahili Forum Na. 19 uk 1-22.

Kirumbi, P. S. (1975) *Misingi ya Fasihi Simulizi*. Nairobi, Shungwaya Publishers.

Kothari, C. R. (2004) *Resaearch Methodology: Methods $ Techniques*. New Delhi: New Age International (P) Limited.

Kneene, M. (2005) *Utenzi wa Hamziyya*. TUKI, Dar es Salaam.

Matteru, M. D. (1983) *Fasihi Simulizi na Uandishi wa Kiswahili III*. Dar es Salaam, TUKI.uk 26-37.

Muhammed, O. (2016) *Mahojiano ya ana kwa ana na Mtafiti*. Khalifa Twariqatul-Qadriya – Zawia ya Msikiti Ngamia Zanzibar. Mei, 18, 2016.

Mulokozi, M. M. (1996) *Fasihi ya Kiswahili*. Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania, Dar es Salaam.

Muhyiddin, A. K. (2015) *Mahojiano ya ana kwa ana na Mtafiti*. Chuo cha Kiislamu, Mazizini - Zanzibar, Juni, 5, 2016.

Mdungi, A. (2011) *Malenga wa Uswahilini*. TAKILUKI, Zanzibar**.**

Mwanamosi, H. (2014) *Mabadiliko ya Kasida Dhima na Uwasilishaji*. Tasnifu ya Shahada ya Uzamili, Chuo Kikuu Cha Dodoma, Tanzania.

Nawaje, A. (2012) *Ufasihi Unaojitokeza katika Kasida za Madrasa*. Tasnifu ya Shahada ya Uzamili, Chuo Kikuu Cha Dodoma, Tanzania.

Nimtz, A. H. (1980) Islamic and Politics in East Africa: The Sufi Order in Tanzania. Minneapols: University of Minnesota Press.

__________ (1971) The Sufi Order in Islam. New York, Oxford University Press.

Nkwera F. (1976) *Tamrini za Fasihi Simulize*: Sekondari na Vyuo. Dar es Salaam University Press: Dar es Salaam.

Ntarangwi, M. (2004) *Uhakiki wa Kazi za Fasihi*. Augustana College, Rock Island, IL 61201.

Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) na Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali (OCGS) Zanzibar (2015). *Sensa ya Watu na Makazi mwaka 2012: Idadi ya Watu kwa ngazi ya Utawala; Matokeo Muhimu.* Dar es Salaam, Tanzania.

Simiyu, F. W. (2011) *Kitovu cha Fasihi Simulizi*. Serengeti Bookshop, Mwanza.

Sengo, T. S. Y. (1992) *Utamaduni wa Kiswahili*. Wilaya ya Kusini Unguja, katika Nordic Journal of African Studies I (i): Kur 53-75.

Senkoro, F. E. M. K. (1985) *Fasihi Simulizi na Mabadiliko.* Mulika juz.17, TUKI, Dar es Salam.

Ww2.al-faqeer. com, Juni 23, 2016.

# VIAMBATISHO

## Kiambatisho I: Orodha ya Mashairi Yaliyotumika Kubainisha Baadhi ya Maudhui ya Ushairi wa Dhikiri

1. Bingwa wa subira    nabii Ayub Mtume
Kavumilia maradhi   yalomkutia Mtume
Wadudu kumbughudhi   yuko kitandani Mtume
Miaka kumi na nane na miezi kadhaa   kavumilia Mtume

2. Ulosema umati bora      tunateseka siyee
Tufanye nini Mola       tufanye nini Mola
Na maasi mengi      yameizama dunia
Huwa ya huwa      huwa ya huwa

3. Msiba ulotufika  umeumbwa na Manani
Yatupasa kukumbuka  waja tulo duniani
Tusije tukaropoka  tukamsahau Manani
Kulia kuomboleza  kwamtoa mtu imani

4. Tujiepushe na balaa la dhulma na ushirikina
Dhambi za mwenye kusengenya sawa sawa na fitina
Halafu Mtume kasema si faradhi wala sunnah
Allah huwaaa

5. Nabi Yunus Mtume Mtume wa Mungu
Mola amemwokoa alipomezwa na chewa
Baharini alikuwa Allah huwa
Marhaba jadal-husain

**Kiambatisho II: Madodoso, Hojaji na Muongozo wa Ushuhudiaji Yaliyotumika Kukusanyia Data za Utafiti**

a) DODOSO KWA WALIMU WA MADRASA, MAKHALIFA, MURIDI NA WATU WAZIMA WANAOJUA KUSOMA NA KUANDIKA

1. Dhikiri ni nini?

…………………………………………………………………………………………

……...........................................................................................................................

.......................................................................................................................................

…………………………………………………………………………………………

……

2. Anayedhikiri anapata nini?

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

…………………………

3. Mambo gani yanayosababisha kuwepo kwa dhikiri?

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

…………………………

4. Ni ipi asili ya dhikiri katika Uislamu?

…………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………

…………………...

5. Uafahamu nini juu ya dhikiri ya asilia?

…………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………

6. Unafahamu nini juu ya dhikiri ya kisasa?

…………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………

7. Kuna aina ngapi za dhikiri? Zitaje.

…………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………

8. Wataje viongozi wa dhikiri unaowajua?

…………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………

…………

9. Unadhani ni mabadiliko gani yanayoikumba dhikiri? Taja matano.

a) ……………………………………………………………………………….

b) ……………………………………………………………………………….

c) ……………………………………………………………………………….

d) ……………………………………………………………………………….

e) ……………………………………………………………………………….

10. Dhikiri hutambwa kulingana na miktadha maalumu.Taja miktadha mitatu.

a) ……………………………………………………………………………….

b) ……………………………………………………………………………….

c) ……………………………………………………………………………….

11. Elezea sababu zilizopelekea kutokea mabadiliko katika dhikiri?

………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………

………………………………

12. Fafanua athari za kuwepo mabadiliko katika dhikiri kwa jamii ya Wazanzibari.

………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………

**ASANTE KWA USHIRIKI WAKO**

b) MWONGOZO WA HOJAJI KWA WALIMU WA MADRASA, MAKHALIFA, MURIDI NA WATU WAZIMA WASIOJUA KUSOMA NA KUANDIKA

1. Dhikiri ni nini?
2. Anayedhikiri anapata nini?
3. Ni ipi asili ya dhikiri katika Uislamu?
4. Kuna aina ngapi za dhikiri? Zitaje.
5. Wataje viongozi wa dhikiri unaowajua.
6. Unadhani ni mabadiliko gani yanayoikumba dhikiri? Taja matano.
7. Dhikiri hutambwa kulingana na miktadha maalumu.Taja miktadha mitatu.
8. Elezea sababu zilizopelekea kutokea mabadiliko katika dhikiri?
9. Fafanua athari za kuwepo mabadiliko katika dhikiri kwa jamii ya Wazanzibari.

**Asante**

c) MUONGOZO WA USHUHUDIAJI

| Mambo ya Kushuhudia | Maeneo ya Kushuhudia | Lengo |
|---|---|---|
| • Hali ya utambaji wa dhikiri na kuona mabadiliko. | Mahali ambapo dhikiri hutambwa. | Kubaini mabadiliko katika dhikiri. |
| • Kuchunguza sababu za kutokea mabadiliko katika dhikiri. | Mahali ambapo dhikiri hutambwa. | Kubaini sababu zilizopelekea mabadiliko katika dhikiri. |
| • Kutathmini athari zitokanazo na mabadiliko ya dhikiri kwa jamii ya Wazanzibari. | Katika jamii ambamo dhikiri hutambwa. | Kubaini athari zinayoipata jamii ya Wazanzibari kutokana na mabadiliko katika dhikiri. |

**Kiambatisho III: Orodha ya Picha.**



***Picha namba 7: Mtafiti (kulia) akimuhoji mwalimu wa madrasat Anfal iliyopo ShauriMoyo Zanzibar (Chanzo: Utafiti, Mei 23, 2016).***



***Picha namba 8: Wanadhikiri wakiwa hawakuvaa sare maalum katika sherehe maalum ya dhikiri huko Tumbatu, Mkoa wa Kaskazini Unguja, Zanzibar (Chanzo: Utafiti, Juni 9, 2016).***



***Picha namba 9: Mtafiti akiwa katika kaburi la Sayyid Omar Qullaten ambaye ni kiongozi wa dhikiri ya Qadiria liliopo Masingini Zanzibar***

***(Chanzo: Utafiti, Juni17, 2016).***



***Picha namba 10: Mtafiti (watatu kushoto aliyesimama ) akiwa katika picha ya pamoja na muridi wa dhikiri katika zawiya ya Msikiti Ngamia, Zanzibar***

***(Chanzo: utafiti, Mei 23, 2016)***

**Tafsiri ya Baadhi ya Maneno ya Kiarabu Yaliyotumika katika Utafiti Huu**

**Dhikiri ya Tasbihi**: Dhikiri ya awali kabla ya kugawanyika matawi.

**Ahlul Tariqa**: Wafuasi wa makundi ya dhikiri.

**Sadaqallahul Adhim**: Ujira wa Mwenyezi Mungu aliye mtukufu.

**Salat al Janaiza**: Sala anayosaliwa aliyekufa (maiti).

**Hizbu Bahr**: Ni kitabu mashuhuri cha dini ya Kiislamu chenye maarifa mengi.

**Humaithira**: Mji mtakatifu uliopo Misri.

**Madrasatul Shadhiliya**: Chuo mashuhuri kinachotoa mafunzo ya dhikiri ya Shadhiliya

**Twariqatul Shadhiliya**: Njia ya wanaofuata dhikiri ya Shadhiliya.

**Ahlul Sunnah wal Jamaa**: Moja ya dhehebu la Kiislamu lenye wafuasi wengi.

**Idhini ya Allah**: Maana yake, kwa amri ya Mwenyezi Mungu